RIPOTI MAALUM

**Kiwanda** chazalisha mifuko iliyopigwa marufuku nchini

UKURASA 4



**Waliotwaliwa** maeneo kuanza kulipwa fidia

UKURASA 5




# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Novemba 5, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581485

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


## MARTINEZ: MBAPPE SHUJAA WA BAADAYE

UKURASA 21



# WABUNGE WAPINGWA

• **Ni** kuhusu sheria vigogo ubadhirifu kunyongwa, wasomi, wanasiasa wawapa somo... *Endelea Ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

### WATAKA KAMATI KUWACHUNGUZA WALIOTAJWA NA CAG



WABUNGE wameshauri kuundwa kamati maalum itakayochunguza ubadhirifu wa fedha uliobainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali...


## Waandamana hadi kwa DC kulalamikia mikopo umiza

UKURASA 3




Kinamama wakijadiliana jambo huku wakiwa wamejikinga mvua kwa mwamvuli, wakati wa kutano wa kumpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa uongozi wake wa miaka mitatu, uliondaliwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), katika viwanja vya Maisara Suleiman, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Mwinyi aahidi makubwa zaidi miaka miwili ijayo

UK. 3


**MICHEZO** **SIMBA, YANGA MECHI YA KISASI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Rais Samia Suluhu Hassan akishiriki Mkutano kuhusu Ulinzi na Usalama (Troika) wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC), jijini Luanda, nchini Angola jana. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo, utajadili juhudi za SADC katika kuimarisha hali ya Amani, Ulinzi na Usalama Mashariki mwa Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). **PICHA: IKULU**

# Wabunge wakosolewa vigogo kunyongwa

**Na Beatrice Shayo**

WASOMI na wachambuzi wa masuala ya siasa wamekosoa mapendekezo ya wabunge kuhusu sheria ya kunyongwa au kukatwa vichwa viongozi wa serikali waliotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusika na ubadhirifu wa fedha za umma.

Pamoja na kukosoa, wametaka kufanyike maboresho ya mifumo iliyopo ili kuwapo na uwajibikaji.

Juzi, bungeni jijini Dodoma, baadhi ya wabunge walipendekeza kunyongwa au kukatwa vichwa kwa viongozi wa serikali, wakiwamo mawaziri na watumishi wa umma, waliotajwa kuhusika na ufujaji na ubadhirifu.

Wabunge hao walisema umefika muda mwafaka wa kuwasilishwa bungeni muswada na sheria ya kutekeleza jambo hilo ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia ya udokozi wa fedha za umma.

Wakizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum kuhusiana na mapendekezo hayo, wadau hao walisema kinachotakiwa kufanyika ni kufanya maboresho katika mifumo iliyopo ili kuwapo kwa uwajibikaji pindi ripoti za CAG zinapotoka.

Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema kauli zilizotolewa na wabunge ni maneno ya kisiasa na hayana maana na kwamba ubadhirifu utaondoka kwa kujenga taasisi imara.

Mchambuzi wa Masuala ya Kiuchumi, Prof. Haji Semboja, alisema ripoti ya CAG huwa inatoa maelekezo lakini tatizo kubwa ni hatua hizo hazifuatwi au kuangaliwa.

"Bunge ni chombo cha kisheria labda walazimishe sheria zilizopo sasa hivi zifanye kazi baada ya ripoti hizo kutoka. Sasa hivi tuna bahati ripoti zinatoka kwa wakati, zamani ilikuwa zinachelewa sana. Lakini kuwahi kwake kunatuonesha kwamba tuna matatizo katika jamii ambayo imeendelea na mifumo yake haiko sawa na hakuna haja kutengeneza sheria nyingi,' alisema.

Prof. Semboja alisema jambo la msingi ni kuboreshwa kwa mifumo ambayo itasaidia kuondokana na tatizo hilo ambapo utaratibu upo na unaeleza nini kifanyike baada ya ripoti ya CAG kutoka.

Alisisitiza kuwa mapendekezo ya wabunge kuhusu kuwapo kwa sheria ya kunyongwa ni ngumu endapo mifumo haitaboreshwa.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Richard Mbunda, alisema ameshangazwa na mapendekezo ya wabunge japo inaonyesha wameumia. Alisema wabunge wamezungumza waziwazi kwa kuashiria kuumia kuona vigogo wanatumia mali za umma wakijua hakuna watakachofanywa.

"Hili bunge limekuwa likibezwa sana kwa maana ya jinsi likiendesha mambo. Mara nyingi lilionekana halikuwa ni bunge la wananchi pengine waliokwenda katika hilo bunge walibebwa na utawala wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Kimsingi wameonekana ni wabunge dhaifu katika mabunge yote tangu mfumo wa vyama vingi ulivyoanza, wapinzani ni wachache ikilinganishwa na miaka mingine ndiyo maana nimeshangazwa na namna walivyozungumza katika hilo," alisema.

Dk. Mbunda alisema mawazo yao ya kutunga sheria kwa ajili ya kushughulia hao ni sahihi, lakini wanatakiwa kujua hawawezi kuitunga kwa ajili ya kuadhibu makosa ambayo tayari yameshafanyika.

Mwanaharakati wa masuala ya kisiasa na kijamii, Bubelwa Kaiza, alisema pengine bunge halijui wajibu wake kwa kuwa lina uwezo wa kufanya uamuzi.

"CAG ni ofisa wa bunge anakagua kwa niaba ya bunge si kwa niaba ya serikali. CAG huwa anakagua serikali, utendaji wake, matumizi ya fedha, kazi na matokeo ya kazi anakagua kwa niaba ya bunge.

Kaiza alisema walitakiwa kuangalia sheria zinasemaje na mamlaka waliyonayo kwa mujibu wa Katiba ili wachukue hatua kwa kuwa mamlaka hiyo ni yao.

## ... Wataka kamati kuchunguza waliotajwa na CAG

**Na Gwamaka Alipipi**, DODOMA

WABUNGE wameshauri kuundwa kamati maalum itakayochunguza ubadhirifu wa fedha uliobainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ili wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Walitoa ushauri huo jana bungeni wakati wakijadili taarifa za Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali (PAC), Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) na Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ambazo ziliwasilishwa bungeni zikichambua taarifa ya ripoti ya CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022.

Mbunge wa Simanjiro (CCM), Christopher Ole Sendeka, alisema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya jitihada mbalimbali kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo lakini inashangaza baadhi wamekuwa wakizitafuna bila huruma.

Alisema hakuna shaka kwamba ripoti ya CAG imethibitisha pasipo shaka matumizi mabaya ya fedha za umma kwa muda mrefu na kwamba kosa liko katika upangaji wa safu ya watendaji na viongozi katika serikali.

Sendeka alitoa rai kukusudia kuwasilishwa marekebisho ya kuliomba bunge kuridhia kuundwa kamati teule ya kuchunguza au kuangalia namna bora ya kufuatilia utekelezaji wa maazimio yanayotolewa na wabunge kuhusu ripoti hiyo na hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliofanya ubadhirifu.

"Namna pekee ya kufanya ni kuunda kamati itakayokwenda kuangalia ukaguzi wa miaka ya nyuma mitatu waliosababisha dosari hiyo wamechukuliwa hatua gani, bado wapo maofisini au wameondolewa.

Tukifanya hivi tutakuwa tumekusaidia wewe (Spika), kuhakikisha bunge linatimiza wajibu wa bunge makini ambalo litaacha rekodi ya kuhakikisha fedha za walipakodi zinafika maeneo kusudiwa," alisema.

Mbunge wa Msalala (CCM), Iddi Kassim, alishauri kuanzishwa chombo maalum kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa umma.

Jafari Chege (Rorya- CCM) alishauri kuundwa chombo maalum cha kufuatilia mwenendo au kesi zinazoendeshwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili hatua zichukuliwe haraka kwa wanaofanya ubadhirifu.

Naye Mbunge wa Bunda Vijijini, Mwita Getere (CCM), alishauri kuundwa kwa kamati ya kufuatilia utekelezaji maazimio ya bunge kuhusu ripoti ya CAG

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Kunti Majala, alishauri kuwa halmashauri ambazo zimeshindwa kufanya kazi ya kukusanya mapato ni vyema watumishi wake wakapumzishwa na kupisha wengine waingie wafanya kazi.

Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe alishauri kurejewa kwa ripoti za CAG za nyuma ili waliofanya ubadhirifu wachukuliwe hatua maana ndio kitu kikubwa ambacho Watanzania wengi wanasubiri.

Pia alishauri kurejewa kwa kanuni za bunge ili ripoti ya CAG inapofika bungeni Machi iendelee kujadiliwa na majibu yawepo wakati wa Bajeti Kuu ya Serikali.

Abdallah Chikota (Nanyamba - CCM) alishauri sheria mamlaka za serikali za mitaa zifanyiwe mapitio ili kuwapa mamlaka baadhi ya viongozi kuwa na nguvu ya kuchukua hatua.

Hata hvyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akitolea ufafanuzi wa kuundwa kwa kamati maalum kwamba ni wazo zuri lakini ni vyema kwa sasa Bunge likaendelea na mfumo uliopo sasa, endapo ikishindikana ndipo Mawazo ya kuundwa kwa kamati maalum itafanyiwa kazi

### HATUA SERIKALINI

Kutokana na suala hilo kuibua msisimko, serikali imesema imechukua hatua na inaendelea kuchukua hatua dhidi ya watumishi wa umme waliotajwa katika ripoti ya CAG kuhusika katika ubadhirifu wa fedha.

Imesema hakuna mtumishi aliyetajwa katika ripoti ya CAG ambaye amehusika katika ubadhirifu atabaki salama, kwamba hadi sasa baadhi yao wameshahukumiwa, wengine kesi zao zipo mahakamani zinaendelea, wengine wamerudisha fedha.

Mawaziri mbalimbali walitoa ufafanuzi huo jana bungeni wakati wakijibu hoja za wabunge waliokuwa wakichangia taarifa ya kamati hizo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema hadi Oktoba, mwaka huu, hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa waliobainika, huku kesi 1,790 zikifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini.

Alisema watuhumiwa 16 waliohusika na kuchukua fedha za POS Sh. bilioni 8.9 walikamatwa, huku Sh. bilioni 5.2 zikirejeshwa serikalini. Alisema hadi sasa kesi 921 zipo katika ngazi mbalimbali mahakamani, kwamba kazi kubwa imefanyika tangu ripoti hiyo itolewe.

Alifafanua kuwa kazi kubwa imefanyika kwa maelekezo ya Rais Samia kwamba TAKUKURU imererejesha Sh. bilioni 14 na Dola za Marekani 14,571.

Simbachawene alisema mali zilizotaifishwa na serikali kutoka kwa wabadhirifu ni za thamani ya zaidi ya Sh bilioni mbili.

Aidha, alisema watuhumiwa 16 wanaodaiwa kuchukua Sh. bilioni 8.9 kati ya Sh bilioni 11 kupitia mfumo wa makusanyo wa POS, wamesharejesha serikalini Sh. bilioni 5.2.

### KITILA MKUMBO

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema suala la kuwafikisha mahakamani wezi wa fedha za umma lilianza muda mrefu na kwamba hakuna waziri anayetetea hoja ya CAG, lakini kuna baadhi ya watu wanataja kiwango kikubwa cha fedha, hivyo kusababisha mkanganyiko wa hoja.

Akijibu hoja ya ubadhirifu katika Mfuko wa Tuzo na Tozo na Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, alisema waliothibitika kutafuna fedha watachukuliwa hatua.

## HABARI KITAIFA

# Waandamana kwa DC kisa mikopo umiza

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

ZAIDI ya wananchi 100 kutoka Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katoro wameandamana hadi ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe, wakilalamika kubambikizwa riba kubwa na kunyang'anywa hati zao za nyumba na mkopeshaji Emanuel Doto, licha ya kumaliza madeni anayowadai.

Wakitoa malalamiko yao baada ya kufika katika ofisi ya mkuu wa wilaya juzi, baadhi ya wananchi hao walisema kilio chao kikubwa ni kubambikiwa riba kubwa na kunyimwa mikataba ya mikopo pamoja na hati za nyumba zao pindi wanapomaliza mikopo na baadaye kudaiwa tena.

Mmoja wa wananchi hao, Beatrice Daudi, alisema walianza kukopa kwa mfanyabiashara huyo tangu mwaka 2016 na kero kubwa ni kuwabambikia riba kubwa na kutowakabidhi hati za nyumba zao pindi wanapomaliza kulipa mikopo.

"Mwaka 2017 nilichukua mkopo wa Sh.600,000 na kufanikiwa kurejesha mkopo huo lakini baada ya miaka miwili nilipigiwa simu na mfanyabiashara huyo akidai kuwa anamdai kiasi cha Sh. milioni 2.4 ilihali nilishamaliza marejesho yangu,"alisema Sevelin Charles mmoja wa waandamanaji hao

Mwenyekiti waandamanaji hao Joseph Masaba alisema kuwa walifuatilia suala hilo hadi Dodoma katika ofisi ya Waziri Mkuu aliyeagiza Mkuu wa Wilaya kulishughulikia suala hili ndipo akakamatwa Mfanyabiashara huyo kisha kuachiliwa bila wao kupewa mrejesho.

"Tumeamua kuandaama leo kujua hatima ya suala letu wananchi wameumia ameachiliwa tena ameanza kufukuza watu kwenye nyumba zao tunaomba tusaidiwe,"alisema Masaba .

Baada ya kusikiliza malalamiko hayo, Magembe aliunda kamati ya watu wanane kuchunguza malalamiko hayo na kuagiza kamati hiyo kuanza kazi yake kesho huku akiwataka wananchi hao kuwa na subira mpaka kamati hiyo itakapokamilisha jukumu hilo.

Magembe alisema serikali inataka kuona wananchi wanasikilizwa na kupata haki zao, hivyo kamati iliyoundwa itawashirikisha maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU, maofisa biashara, wanasheria, polisi, na vyombo mbalimbali vya dola.

Alisema kila mmoja atahojiwa ili kuhakikisha kila upande unapata haki huku akiwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa kamati hiyo.

"Kamati hii itafika kwenye mahakama, wenyeviti, maofisa watendaji wa mitaa na kuwahoji walalamikaji na mfanyabiashara huyo ili kujiridhisha na haki itendeka kwa pande zote mbili," alisema.

Magembe alisema baada ya kupokea maelekezo kutoka kwa Waziri Mkuu, mfanyabiashara huyo alishikiliwa kwa ajili ya hatua za kisheria na ofisi ya mwendesha mashtaka ilifungua na kesi kwa namna ambayo ilikuwa imefunguliwa, mfanyabiashara huyo hakustahili kupata dhamana lakini waliamuwa kuliondoa kwanza shauri hadi ushahidi utakapokamilika.

Mkuu huyo aliongeza kuwa uchunguzi wa awali, alipokamatwa mfanyabishara huyo, ulibaini kuwa biashara ya ukopeshaji wa fedha alianza toka mwaka 2011 na amesajili kampuni ya ukopeshaji (Kapaya Microfinance) mwaka 2022.

Wakili wa mfanyabiashara huyo, Beatus Emanuel, aliiambia Nipashe kuwa malalamiko hayo yapo na akadai kwamba baadhi yao waliokuwa wakidaiwa wameshafikishwa mahakamani kutokana na kampuni hiyo kufanya kazi kwa mujibu wa sheria lakini malalamiko hayo yanaweza kumalizika kwa mazungumzo.

# Mwinyi aahidi makubwa zaidi miaka miwili ijayo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ataendelea kujituma kwa ajili ya maendeleo ya nchi na kutumia nguvu zake zote kuhakikisha anawaondoa Wazanzibar katika umaskini.

Vilevile amesema atahakikisha anatimiza ahadi zote zilizopo katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Akizungumza katika sherehe za kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake tangu alipopewa dhamana ya kuongoza Zanzibar Novemba 3, 2020, Rais Mwinyi aliwaomba wananchi kuendelea kumuunga mkono ili kutimiza malengo hayo.

Sherehe hizo ambazo zimeandaliwa na Umoja wa Wanawake wa CCM Tanzania (UWT) zilifanyika katika viwanja vya Maisara na kuhudhuriwa na watu mbalimbali.

Rais Mwingi pia aliwaomba wananchi kuendelea kuhubiri amani na utulivu wa nchi kwa sababu bila ya hayo maendeleo hayatopatikana.

Alisema kwa kuliona hilo ndio maana alipoingia madarakani, kwa makusudi akafanya mazungumzo na chama cha upinzani na kuweka Serikali ya Umoja wa Kitaifa na anafarajika hadi sasa kuona kuna amani na utulivu wa kutosha.

Katika kipindi kilichobaki cha uongozi wake wa miaka miwili, alisema kasi yake itakuwa kubwa zaidi ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa bandari ya Mangapwani ambao utagharimu karibu Dola milioni 400 na ujenzi mkubwa wa uwanja wa ndege Pemba.

"Ninataka niwaahidi kwamba 2025 yale tuliyoyaahidi tutakuwa tumeyatekeleza kwa kasi ya aina yake kuanzia sasa katika kipindi cha miaka miwili hii iliyobaki,"alisema.

Rais Mwinyi alipongeza UWT kwa hamasa, kutembelea miradi ya maendeleo ya ufuatiliani wa utekelezaji wa ilani ya CCM na kuishukuru CCM kwa kuendelea kumuunga mkono katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Alisema yako maeneo ambayo ameshamaliza kutekeleza ilani ya CCM ikiwamo katika sekta ya elimu, hivyo hana wasiwasi ya kwamba 2025 atatembea kifua mbele katika majukwaa ya kisiasa kwa sababu, atakuwa ametimiza yale aliyoahidi.

"Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Rais Samia (Suluhu Hassan) kwa msaada wake mkubwa kwangu kila mara tukipata changamoto mbalimbali ninakwenda kwake, hakuna hata mara moja ambayo hakuniunga mkono kutimiza yale ambayo yapo ndani ya uwezo wake.

"Mengi katika tuliyoyafanya hapa Zanzibar yana mkono wake amenisaidia katika kupata fedha za kutekeleza mambo mengi. Katika miaka mitatu ya uongozi wangu, nimefarijika kuona wapo wengi wanaothmini mambo ninayoyafanya, kwa sababu wakati mwingine katika kazi ya kuiongoza hupata sonono kwa kujituma, lakini mengi unayoyasikia ni lawama na malalamiko," alisema.

Mwenyekiti wa Taifa wa UWT, Mary Chatanda, alisema utekelezaji wa ilani ya CCM ni mzuri katika sekta zote kwa sababu wameshuhudia miradi mingi iliyotekelezwa.

Alitaja baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa masoko, barabara, shule, hospitali za kisasa na miradi ya maji.

Alisema wanawake wa Zanzibar wamekiri kupatikana kwa huduma ya maji hali ambayo imesababisha ndoa zao kuimarika maana sasa hawaendi kufuata maji alfajiri.

Mwenyekiti huyo alimpongeza kwa maboresho makubwa katika huduma ya maji kwa kuchimba visima na kupunguza muda mkubwa kwa wanawake kutafuta maji na sasa wanapata muda wa kushiriki shughuli za kiuchumi.

Alisema wamefanya ziara katika mikoa yote ya Zanzibar na miongoni mwa waliofanya ni kuwahamasisha wanawake wenye sifa kujitokeza kugombea katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, kukemea suala la kuporomoka kwa maadili na kukemea vitendo vya udhalilishaji.

Alisema Rais Mwinyi amewezesha sekta ya utalii kwa kuvutia wawekezaji kuwekeza na kutengeneza ajira kwa vijana ikiwamo wanawake.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 93 YA 2023**
**OMARY K.UREMBO..................MLETA MAOMBI**
**OMARY KIBWANA UREMBO......MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**RUANDA L. SENGO, SHABANI MABULA, RUKIA RASHIDI, ZAITUNI ABDALLAH@MWANAHAWA CHAGIMALE, KIBWANA KIDEHELE......WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA SHABANI MABULA**
Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 20/11/2023 mbele ya mwenyekiti E.MOGASA wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 19 Mwezi Oktoba 2023.

......................................
**M.MOGASA**
**MWENYEKITI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1963 NYONGEZA YA 5 FASILI NA 2)**
**Mbele ya Mahakama ya mwanzo ya Mjini Tanga**
**Usimamizi wa Mirathi ya...Mwinyikombo Shali**
**Mirathi No...91/2008**

Mnamo leo...2/6/2017.....Mbwana Mwinyikombo ameteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Mwinyikombo Shali ambaye amefariki mwaka 1976 akiwa ameahidi kusimamia mirathi hiyo kwa wema na uaminifu kama iliyovyoelezwa hapo chini.
Mirathi isimamiwe na kufuata nakala ya wasia wa marehemu unaoambatanishwa.
Imetiwa sahihi leo 2/6/2017.
Mimi nathibitisha kwa kiapo hiki kuwa nitasimamia kwa wema na uaminifu Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu nitalipa madeni yake ya haki na kugawa haki ya mirathi yake kwa mujibu wa sheriaa. Nami nitaweka hesabu kamili na za kweli ya mali yote ya mirathi ya marehemu na jinsi nitakavyofanya hivyo. Nami nitaonesha hesabu hiyo mbele ya Mahakama hii siku yoyote zitakapotakiwa.
Imetiwa sahihi leo 2/6/2017.

..........................
**MSIMAMIZI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MUFINDI**
**Kituo cha MAFINGA Mkoa IRINGA**
**Shauri la madai Na 39/2023**
**Jina la mdai..................MUCOBA BANK PLC**
**Jina la Mdaiwa............WASHINDI GROUP GANGILONGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa WASHINDI GROUP GANGILONGA**
Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (eleza hapa habari za madai) **MADAI YA TSHS.2,637,000/= YATOKANAYO NA MKOPO KUTOKA MUCOBA BANK PLC**. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa 8:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**Tarehe 03/11/2023**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe **06-11-2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DER ES SALAAM** kuelekea **DODOMA,** gari hilo lenye namba za usajili:

**T 175 DFN / T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18.00**
**Upana - mita 2.80**
**Kimo - mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **DODOMA** kupitia **MOROGORO**.
Gari itasafiri muda wa mchana tu (**kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

# Kiwanda chazalisha mifuko iliyopigwa marufuku nchini

## - Shehena kubwa yanaswa; TRA, NEMC watoa angalizo

**Na Halfani Chusi**

KIWANDA kilichosajiliwa kuzalisha mifuko yenye ubora kwa ajili ya kubebea bidhaa, kimebainika kuzalisha mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na serikali tangu mwaka 2019.

Kiwanda hicho kilichoko Mbezi Juu, wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, kinamilikiwa na kampuni ya Toco & Company Limited inayomilikiwa na raia wa China. Ilisajiliwa nchini Oktoba 19, 2019.

Juni Mosi, 2019 serikali ilianza kutekeleza rasmi marufuku ya kuzalisha, kusambaza na kutumia mifuko ya plastiki, hivyo Kampuni ya Toco & Company Limited ilisajiliwa nchini miezi minne baada ya hatua hiyo ya serikali.

Kutokana na kubainika kwenda kinyume cha sheria na maelekezo ya serikali, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Sadi Mtambule, alibainisha juzi kwamba walikifunga kiwanda hicho baada ya ziara ya kushtukiza kiwandani hapo na kukuta shehena ya mifuko hiyo.

Juzi asubuhi, Nipashe ilifika eneo hilo na kushuhudia kiwanda kikiwa kimefungwa huku baadhi ya wafanyakazi wakiwa nje kusubiri hatima yao huku nje ya kiwanda hicho kukiwa na bango linaloonyesha kinazalisha mabati.

Mtambule alisema wamekamata baadhi ya viongozi wa kiwanda hicho kwa ajili ya mahojiano na hatua zaidi za kisheria.

"Hatua tulizozichukua ni pamoja na kufunga kiwanda hiki na tunasaka stoo zingine ambazo wamehifadhi mifuko hii. Tunaangalia sheria inatuelekeza nini; tufunge moja kwa moja au apigwe faini na kupewa muda wa kujirekebisha.

'Tulichokiona ni kwamba ana leseni mbalimbali zinazomtaka kuzalisha mifuko ya plastiki yenye ubora, lakini yeye anafanya kinyume.

Mifuko anayozalisha ni ile iliyopigwa marufuku mwaka 2015 (utekelezaji ulianza rasmi kisheria Juni Mosi 2019). Kwa sasa wanajifanya wajanja, wanatoa yenye rangi ya bluu ambayo mwanzoni ilikuwa ina rangi nyeusi," alifafanua.

Mtambule alisema walipata taarifa kuwapo mifuko hiyo mtaani, lakini hawakujua anayeizalisha mpaka walipopewa taarifa na raia wema kuhusu kinachoendelea katika kiwanda hicho.

"Njia nyingine iliyotusaidia ni kutumia macho mengine ya serikali ya kutupatia taarifa. Wanatumia ujanja sana, wanazalisha wikiendi na usiku na hata wanavyoisambaza huwezi kumjua mhusika moja kwa moja.



Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo


Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule

"Soko lao kubwa ni kwa wenye bucha na sokoni. Wakati tunaingia kiwandani, kuna lori tulilikamata limebeba hiyo mifuko, lilikuwa linaipeleka Ilala ili ikasambawe kwa wanaoihitaji," alisema huku akibainisha kuwa uchunguzi umebaini kuwa kwa siku kiwanda hicho kinazalisha mabando 60 ambayo kila moja lina zaidi ya mifuko 2,500 na usafirishaji wa biashara hiyo hufanywa usiku, hivyo si rahisi wahusika kugundulika.

Mkuu wa Wilaya alisema tayari wameelekeza mamlaka zingine zikiwamo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zichukue hatua dhidi ya wamiliki kwa mujibu wa sheria za nchi.

### MADHARA YAKE

Meneja wa NEMC Kanda ya Kaskazini Mashariki, Glory Kombe, alithibitisha kuwa walipozuru kiwandani hapo, walibaini kinazalisha mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku kutokana na madhara yake kiafya na mazingira.

Kombe alisema baraza limefanya ukaguzi na kutoa matangazo kwamba viwanda vinavyozalisha vifaa vya plastiki ni lazima visajiliwe kwao ili iwe rahisi kuvifuatilia.

"Lakini kiwanda hiki hakikufanya hivyo wala hakina EIA (Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira) na kinazalisha mifuko ambayo ina athari kwa mazingira na afya. Kwa hiyo, sisi NEMC tunakifunga kiwanda hiki mpaka pale tutakapokubaliana kwa mujibu wa taratibu za kisheria," alisema.

Alibainisha kuwa mifuko hiyo ina athari kubwa kwa mazingira kwa kuwa haiozi, inakaa zaidi ya miaka 500 bila kuoza na inaweza kuharibu afya ya udongo na mifumo ya ikolojia. Alisema inaziba mito na miundombinu ya madaraja na mifereji ya kupitisha maji. Kwa baharini, alisema inaweza kuua viumbe wakiwamo samaki.

"Athari za mifuko hiyo kwa binadamu ni pamoja na kusababisha saratani hasa inapotumika kubeba vyakula vya moto kwa kuwa ina tabia ya kuacha kemikali.

Pia tumebaini katika uzalishaji wake, inatengenezwa kwa kurejelezwa taka zilizokusanywa. Kwahiyo, si rahisi kujua taka za mwanzo zilikuwa na athari gani kiafya na mazingira," alisema.

### MAJIRANI WANENA

Rehema Bakari, mkazi wa eneo kiliko kiwanda hicho, alisema kwa muda mrefu amekuwa anashuhudia baadhi ya magari yakiingia usiku kuchukua mzigo.

Mkazi mwingine, Mariam Komba, pia alisema amekuwa anashuhudia mifuko hiyo ikizalishwa eneo hilo ingawa mtaani kwao haiuzwi. Akawa na fikra kwamba inauzwa mbali kwa kuhofia wenyeji wangeirifu serikali.

"Tangu walipofungiwa juzi hatujaona lolote linaendelea. Serikali ichukue hatua stahiki kwa sababu ile mifuko ina madhara makubwa sana kwa wanyama kama ng'ombe na mbuzi na hata sisi binadamu," alisema.

naye Juma Bakari, mkazi wa Wazo, alisema kiwanda hicho ni cha muda mrefu na uzalishaji huo umekuwa unafanyika tangu mwaka 2019, yaani miaka minne iliyopita.

### WAFANYAKAZI

Baadhi ya wafanyakazi wa kiwanda hicho waliozungumza na mwandishi na kuomba hifadhi ya majina yao, waliomba serikali hatua zichukuliwe haraka ili wajue hatima yao.

"Ni kweli tulikuwa tunazalisha mifuko ya plastiki ile yenye rangi ya bluu, lakini tulipokuwa tukihoji, walituambia hii yenye rangi ya bluu imekubaliwa," walidai wafanyakazi hao huku wakisema tangu kufungwa kwa kiwanda hicho, hawajui kinachoendelea.

"Hapa hakuna tunachojua, tunasubiri uamuzi wa serikali, walikuja jana (juzi) na kundi la watu wakiwamo polisi na watu kutoka NEMC, wakasema tunazalisha mifuko ambayo ilipigwa marufuku na serikali.

"Wakaondoka na baadhi ya mabosi wetu. Kwahiyo, mpaka sasa hatujapata mrejesho wowote," alisema mmoja wa wafanyakazi hao aliyedai kiwanda hicho kina wafanyakazi 20 walioajiriwa (wanawake 12).

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo, alipotafutwa na mwandishi juzi kuzungumzia suala hilo, alisema: "Tunafanyia kazi maagizo ya serikali. Kwa sasa suala hili linashughulikiwa kwa taratibu zetu za ndani, taratibu zetu haziruhusu kuweka wazi taarifa za mlipakodi," alisema Kayombo.

### USULI, ADHABU

Mnamo Juni Mosi, 2019, serikali ilitangaza kisheria kuwa ni kosa la jinai kutengeneza, kuagiza, kusambaza na kutumia mifuko ya plastiki nchini. Wote watakaokaidi marufuku hiyo watakutana na adhabu.

Marufuku hiyo inahusisha maeneo yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Hatua hiyo pia imeshachukuliwa na nchi jirani za Rwanda na Kenya.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004) ilifanyiwa marejeo katika kanuni zake mwaka 2019, kukiingizwa kifungu cha kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki.

Kifungu cha nane cha kanuni hizo kinaorodhesha makosa matano ambayo ni; kuzalisha na kuagiza mifuko ya plastiki, kusafirisha nje ya nchi mifuko ya plastiki, kuhifadhi na kusambaza mifuko ya plastiki, kuuza mifuko ya plastiki na mwisho kumiliki na kutumia mifuko ya plastiki.

Kila kosa lina adhabu yake kwa mujibu wa kanuni hizo kulingana na uzito wa kosa lenyewe.

Kwa kosa la kwanza la uzalishaji na uagizaji adhabu yake ni: Faini isiyopungua Sh. milioni tano na isiyozidi Sh. milioni 20; kifungo kisichozidi miaka miwili gerezani; au mjumuiko wa adhabu zote mbili za awali - faini na kifungo.

Adhabu za kosa la pili ambalo ni kusafirisha mifuko nje ya Tanzania ni sawa na za kosa la kwanza.

Kwa kosa la tatu la kuhifadhi na kusambaza mifuko adhabu zake ni: Faini isiyopungua Sh. milioni tano na isiyozidi Sh. milioni 52; kifungo kisichozidi miaka miwili; faini na kifungo kwa pamoja.

Ukipatikana na hatia ya kuuza mifuko ya plastiki adhabu ambazo utakumbana nazo ni: Faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 500,000; kifungo kisichozidi miezi mitatu gerezani au adhabu zote mbili za awali - kifungo na faini.

Kutumia na kumiliki mifuko ya plastiki kuanzia Juni Mosi, 2019 nchini, utalipa faini isiyopungua Sh. 30,000 na isiyozidi Sh. 200,000, kifungo kisichozidi siku saba gerezani au faini na kifungo kwa pamoja.



Lango kuu la kiwanda kilichofungiwa kuzalisha mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na serikali, likiwa limewekwa bango linaloonyesha kuwa kinashughulika na uzalishaji wa mabati. **PICHA: HALFANI CHUSI**

HABARI KITAIFA




Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Morogoro (Uzalishaji), Dk. Rosalia Rwegasira (wa tatu kushoto), akikabidhi cheti cha pongezi kwa mmoja wa wakulima wa miwa wa Kilombero, Bakari Mkangamo kwa kuchangia maendeleo ya wakulima wa miwa, wakati wa kilele cha Maonyesho ya Siku ya Wakulima wa Miwa Kilombero katika viwanja vya TEM Kilombero hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliotwaliwa maeneo kuanza kulipwa fidia

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa amesema kuanzia wiki ijayo Halmashauri ya Jiji la Dodoma itaanza kulipa fidia wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa na tayari Sh.Bilioni 4.5 zimetolewa na serikali kwa ajili hiyo.

Aidha, ametangaza kupiga kambi na wataalamu wake kwenye Jiji hilo kuanzia jana ili kutekeleza maelekezo ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kutatua migogoro ya ardhi.

Akizungumza jana kuhusu kliniki ya ardhi iliyoandaliwa na Wizara hiyo kwa kushirikiana na Jiji, Silaa alisema wananchi wanaodai fidia ya viwanja Jiji hilo limeanza kupima ili wapewe.

"Kuanzia wiki ijayo Mkurugenzi wa Jiji ameshapata fedha za fidia ana Sh.Bilioni 4.5 kulipa wananchi fidia ambao maeneo yao yametwaliwa ili upimaji wa ardhi uanze," alisema.

"Tukiri kupokea maelekezo ya chama na tumeanza kuyatekeleza, pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Wizara lakini tuongeze kasi, leo tunazindua kliniki nyingine tena Jiji la Dodoma. Kuna maelekezo yalitolewa na Waziri Mkuu kupitia kamati iliyokuwa imeundwa na tumeanza kutekeleza, Dodoma kwasasa ni Mkoa maalum wa Ardhi na tunaye Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dodoma," aliongeza.

Alisema wamejipanga kuhakikisha matatizo ya ardhi Dodoma yanakwisha na yaliyopo nchini na kunafanyika mabadiliko ili watanzania wasiwe na kero sekta ya ardhi kulingana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia alisema wizara na jiji wanaandaa eneo ambalo litakuwa kituo cha kutoa huduma kwa pamoja zote za ardhi ikiwamo upatikanaji wa hati miliki.

"Ofisi zetu zitakuwa za kisasa pale ambapo haihitajiki kuweka vyumba vyumba vingi maeneo yatakuwa wazi kwenye huduma ili watu wasijifungie na wateja ofisi kuwaomba rushwa, na ili kuongeza uwazi zitafungwa kamera ili Katibu Mkuu afuatilie kwa karibu," alisema.

Silaa alisema kliniki hiyo ya ardhi haitakuwa na mwisho hadi matatizo ya ardhi Jiji la Dodoma yaishe na baada ya zoezi hilo kutakuwa na ofisi za kisasa zenye kamera.

Aidha, alimuagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuhakikisha wataalamu wa maeneo yote nchini watoke maofisini wahudumie watu kwa uwazi.

"Mimi kuanzia Jumatatu nikitoka bungeni saa 8:00 mchana nakuwa hapa kusikiliza kero za wananchi ambazo zinahitaji zisikilizwe na Waziri tu, na nimeelekeza ofisi zote za ardhi wataalamu watoke na kliniki kama hii iwe kote nchini,"alisema.

Naye, Mmoja wa wananchi, Asha Abdallah alimshukuru Waziri kwa kuanzisha kliniki hiyo na kushauri iwepo kila wiki kusikiliza wananchi kwa kuwa wanakabiliwa na matatizo ya ardhi.

Hivi karibuni, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Paul Makonda alitoa maelekezo ya chama kwa Waziri Silaa ya kupewa miezi miwili hadi Desemba 31, 2023 kutatua migogoro ya ardhi Jiji la Dodoma.

# Bandari Kwala yaanza kuhudumia EAC, Kusini

**Na Restuta James**

TANZANIA imeanza kuhudumia nchi za Afrika Mashariki, Kusini na Kati kupitia bandari kavu ya Kwala, ili kurahisisha mizigo kuingia na kutoka kwenye mataifa hayo.

Aidha, imetenga hekta 100 katika bandari kwa ajili ya nchi hizo zinazotumia bandari ya Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya kikazi katika bandari ya Kwala juzi,

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara, alisema lengo la kushawishi kutumia bandari hiyo kavu ni kwa kuwa mifumo yote ya kiforodha iko tayari na inasomana.

Alisema mizigo hasa inayosafirishwa nje ya nchi itahudumiwa kwa urahisi katika bandari hiyo na kwamba mawaziri wa miundombinu na usafirishaji kutoka nchi za Ushoroba wa Kati wanatarajiwa kukutana mwishoni mwa mwezi huu kujadiliana namna kufanya biashara ya usafirishaji katika nchi hizo.

Profesa Kahyarara alitaja nchi hizo kuwa ni Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kwamba nchi za Malawi na Zambia zimeomba kuwa mwanachama wa ushoroba huo.

Alisema takwimu za uchumi zinaonesha kwamba sekta ya usafirishaji inaiingizia nchi fedha nyingi za kigeni ikichuana na utalii pamoja na madini, hivyo bandari ina nafasi ya kuongeza mapato ya nchi kupitia usafirishaji wa mizigo.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuhakikisha Tanzania inatumia vizuri fursa yake ya kuwa na bandari kuhudumia nchi zisizo na bandari.

"Unapokuwa Kwala huna sababu ya kwenda Bandari ya Dar es Salaam. Tuna meli nyingi zinakuja na tuna wateja wengi sana. Maombi ni mengi na matarajio ya wateja ni makubwa pia.

Kwala imeunganishwa na reli hivyo mizigo inaletwa hapa kwa treni na huduma zote za kiforodha zinafanyika hapa," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Meneja wa Bandari ya Kwala, Alexander Ndibalema, alisema bandari hiyo ina ukubwa wa hekta 502 na kwamba 100 zimetengwa kwa ajili ya nchi zinazotumia bandari ya Dar es Salaam.

Ndibalema alisema hekta tano zimeshaendelezwa na zimeanza kuhudumia wateja baada ya mifumo yote ya kiforodha kukamilika na inaweza kuhudumia makasha 3,500 kwa wakati mmoja.

# Wakulima tumbaku kuvuna tani 210,000

**Na Joseph Mwendapole**

WAKULIMA wa tumbaku kwenye mikoa mbalimbali nchini wanatarajia kuzalisha tani 210,000 katika msimu wa mwaka 2023/2024.

Hayo yalisemwa hivi karibuni jijini Dar es Salaam na Meneja Mkuu wa Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Wakulima wa Tumbaku (TCJE), Benedict Kisaka, kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 35 wa Umoja wa Wakulima wa Tumbaku Duniani (ITGA).

Alisema mkutano huo wa nchi wanachama umehudhuriwa na wawakilishi kutoka nchi wanachama ambazo ni Argentina, Brazili, Bulgaria, Zambia, Malawi, Zimbabwe, Poland, Ureno, Afrika Kusini, Marekani na Hispania.

Alisema kwenye mkutano huo watazungumza kuhusu kilimo endelevu cha tumbaku na kwamba mwezi ujao Shirika la Afya Duniani (WHO) limeandaa mkutano nchini Panama kuhusu namna ya kudhibiti matumizi ya tumbaku.

Wanachama wa ITGA, ALISEMA watashiriki kwenye mkutano huo na kwamba moja ya ajenda ambazo wakulima watawasilisha kwenye mkutano huo ni hali ya kutokuwa na usawa katika sheria zinazowabana wakulima wa tumbaku kwenye kuendeleza zao hilo.

"Kwa sauti moja na mada zilizowasilishwa kwenye mkutano huu tutaangalia Sera za kumlinda mkulima wa tumbaku na tutashirikiana kujua jitihada zinazofanywa kupunguza uzalishaji wa tumbaku," alisema

Alisema washiriki wa mkutano huo watapata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali yanayozalisha na kuchakata zao la tumbaku ili waone namna Tanzania inavyofanya.

Kisaka alisema tumbaku ni miongoni mwa mazao matano ya kimkakati nchini Tanznaia na kwamba zao hilo linalimwa na wakulima milioni 2.5.

Alisema zao hilo linaiingizia Serikali Dola za Marekani milioni 182 kila mwaka kwa mauzo ya nje ya nchi na kwamba mchango wa zao hilo kwenye uchumi umekuwa ukiongezeka kila mwaka.

Alisema wamekuwa wakifanya jitihada za kuboresha zao hilo ambapo kwa mwaka 2021/2022 walifanikiwa kuzalisha kilo milioni 62 kwa mwaka na mwaka uliofuata 2022/2023 tani 138,000 na kwamba kwa msimu wa 2023/2024 wanatarajia kuzalisha tani 212,000.

Alisema China ndiyo inaongoza duniani kwa mahitaji makubwa ya tumbaku na kuongeza kuwa wamekuwa wakilima kwa wingi kukidhi masoko ya nchini humo

"Soko la tumbaku ni kubwa na kwa bahati nzuri hata kabla mkulima hajaanza kulima anakuwa ameingia mkataba na kampuni za kununua zao hilo kwa hiyo inakuwa rahisi kwa mkulima kuwa na uhakika wa soko na kulima kisasa," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa ITGA, Mercedes Vazquez, ambayo makao yake makuu yako Ureno, alisema umoja huo una wakulima wa tumbaku zaidi ya milioni 40,000 duniani kutoka katika nchi 22.

Alisema wanachama wa umoja huo wako hapa nchini kujadili namna ya kuongeza uzalishaji huo kwenye nchi zinazolima zao hilo.

"Mwezi ujao WHO watakuwa na mkutano nchini Panama kujadili kuhusu kupunguza uzalishaji wa tumbaku tutachukua miongozo ya shirika hilo na kuifanyia kazi ili kuona namna tunavyoweza kuendelea kuzalisha tumbaku lakini tukizingatia miongozo ya WHO," alisema.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Shinikizo hili la wabunge liwaamshe watu usingizini

**BUNGE** ambalo linaendelea na mkutano wake wa 13 jijini Dodoma, juzi na jana lilitawaliwa na mjadala mkali kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka ulioishia Juni, 2022. Mjadala huo ulitokana na taarifa zilizowasilishwa na kamati za bunge za Hesabu za Serikali (PAC), Mitaji na Uwekezaji wa Umma (PIC) na Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Ripoti hizo zilizowasilishwa na wenyeviti na makamu wenyeviti wa kamati hizo, zilibainisha kuwapo kwa ubadhirifu wa mabilioni ya fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kubainishwa kwa ubadhirifu huo uliofanywa na baadhi ya maofisa wa serikali, baadhi ya wabunge walijadili kwa kina na kupendekeza kwamba uwasilishwe bungeni muswada wa sheria ili wale wote wanaotajwa katika ripoti za CAG, ambazo madudu hayo yamekuwa yakijirudia kila mwaka, wachukuliwe hatua zikiwamo za adhabu ya kunyongwa pindi vyombo vya sheria vitakapobainisha kuwa wamefanya makosa.

Miongoni mwa wabunge waliochangia taarifa hizo, walisema kila mwaka inapotolewa ripoti ya CAG, kumekuwa na ubadhirifu wa mabilioni ya Shilingi ambayo yanaelekezwa katika miradi lakini cha kushangaza, fedha zinaingia katika mifuko ya wajanja huku wananchi wakiendelea kukosa huduma muhimu. Kutokana na hali hiyo, walisema ni wakati mwafaka kwa watu hao kushughulikiwa ipasavyo huku baadhi ya mawaziri wakitajwa kuwa sehemu ya matatizo hayo.

Hata hivyo, kauli hizo za wabunge zimepingwa na baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa na wasomi kwamba hatua hiyo haitasaidia bali kinachotakiwa ni kutengeneza mfumo ambao utawawajibisha wale wote wanaotajwa kuhusika na ubadhirifu huo.

Kilio cha wabunge hao ni kutokana na ukweli kwamba kila mwaka taarifa za CAG zimekuwa zikionyesha madudu ndani ya wizara na taasisi za serikali lakini hakuna hatua za wazi zinazoonekana kuchukuliwa dhidi ya wahusika. Kama wako wanaochukuliwa hatua, ni 'dagaa' huku 'mapapa' na manyangumi yakiachwa yakitamba.

Pamoja na kwamba kauli hizo zimepata upinzani, ni wakati wa watu wanaotajwa kujitafakari kwa sababu wahenga wanasema lisemwalo lipo, kama halipo linakuja. Kuna uwezekano mkubwa miaka ijayo au wakati wowote kuanzia sasa, mapendekezo hayo yakafanyiwa kazi kwa sheria kutungwa.

Hilo liko wazi kutokana na muundo wa sasa wa bunge ambao kwa asilimia kubwa una wabunge kutoka chama tawala. Mazingira pia yanaonyesha kuwa jambo lolote ndani ya bunge, huanza taratibu na hatimaye sheria kutungwa. Mfano ni muswada wa sheria ya kulipwa kwa wenza wa viongozi ambao umepitishwa wiki hii lakini ulianza kama utani kwa mwenza mmoja wa viongozi kutoa wazo.


Aidha, kadiri mambo yanavyoendeshwa ndani ya chombo hicho cha kutunga sheria, imeshuhudiwa sheria mbalimbali zikitungwa zikiwamo kandamizi ambazo zimelalamikiwa na sasa zimeanza kufanyiwa marekebisho.

Moja ya sheria ambazo zimepigiwa kelele na wadaawa ni ile Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016. Kama sheria hiyo ilitungwa, nini kitashindikana kama utawasilishwa muswada wa kutungwa kwa sheria ya wabadhirifu na mafisadi wa fedha za umma kunyongwa?

Pamoja na yote hayo, ni dhahiri kwamba kauli hizo za wabunge hazina ishara njema kwa siku zijazo. Ni vyema watu wanaopewa madaraka kutafakari kwa kina na kubadilika kwa kuwa lolote linawezekana na miongoni mwao wakawa waathirika iwapo sheria hiyo itatungwa kama wabunge wanavyotaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

### Vita dhidi ya biashara ya madanguro isiishie Kinondoni

**MACHI,** mwaka huu, Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, alianzisha operesheni kupambana na biashara ya madanguro kwenye eneo lake la utawala.

Katika operesheni hiyo iliyofanyika Mwananyamala, aliitolea ufafanuzi kwamba ilikuwa ya kukusanya taarifa za maeneo yanayofanya biashara hiyo na kisha akawaita wamiliki wa nyumba waliobadili kuwa vyumba vidogo vya kupangisha madada poa na kuwapa onyo.

Aidha, akiwa katika msako wa madanguro eneo la Mwananyamala, akabainisha kugundua madanguro 320 ndani ya manispaa yake, katika maeneo ya Mwananyamala, Tandale na Msasani.

Katika ufafanuzi wake Mstahiki Meya huyo kuhusu madanguro hayo, alisema Mwananyamala yako 150, Tandale 135 na Msasani 35 na kufafanua kuwa vita aliyoianzisha dhidi ya madanguro hayo ni endelevu.

Nikirejea kwenye hoja yangu ni kwamba, wakati Songoro na timu yake wakipambana na biashara ya madanguro, ninadhani ni vyema viongozi wengine kuiga mfano huo, ili vita hiyo iwe na mafanikio.

Iwapo viongozi wote katika maeneo yao ambayo kuna biashara hiyo watachukua hatua za kupambana nayo kama ambavyo wa Kinondoni wanafanya, inaweza kuwa rahisi kumalizika.

Lakini pia si vibaya kutafuta mzizi au chanzo cha kuwapo kwa biashara hiyo, ili kuweka mikakati ambayo inaweza kudhibiti chanzo chake na kuimaliza, wahusika wajishughulishe na biashara halali.

Kwa nini? Kwa sababu biashara ya madanguro ni ya miaka nenda miaka rudi, na baadhi ya watu waliwahi kusikika katika msako huo wa kwanza wa Mstahiki Meya wakidai hayo ndio maisha yao ya kila siku.

Inawezekana wakawa na hoja, ingawa ukweli, lakini ugumu wa maisha hauwezi kuhalalisha biashara hiyo, bali watafutiwe njia nzuri ya kuishi bila kufanya biashara hiyo, ambayo kimsingi inadhalilishan utu wao.

Ninaamini zipo shughuli nyingi za kufanya ambazo zinaweza kuwaingizia kipato, lakini mazoea na kutafuta fedha kwa njia zisizo halali ndio yanayochangia wengi kuingia kwenye biashara hiyo.

Siku nne zilizopita, Mstahiki Meya aliendeleza operesheni ya kutokomeza madanguro huku baadhi ya dadapoa wakikamatwa na wengine kutimua mbio kukwepa kukamatwa na vyombo vya dola.

Lakini anarusha dongo kwa baadhi ya viongozi wa serikali na baadhi watendaji kwamba wananufaika na biashara hiyo, huku akisema hawezi kurudi nyuma katika mkakati wa kupambana nayo.

Kwa kuwa ameamua kupambana na biashara hiyo, jambo la msingi aigwe na maeneo mengine ya Dar es Salaam katika vita hiyo, lakini pia kitafutwe chanzo cha kuwapo biashara hiyo ili vita iwe na mafanikio.

Njia hiyo inaweza kusaidia wahusika wasiwe na mahali pa kukimbilia, lakini pia wanaweza kuelekezwa kufanya biashara nyingine halali za kuwaingizia kipato, badala kujidhalilisha kwa kuuza miili yao.

Iwapo vita hiyo itabaki Kinondoni tu, wahusika wanaweza kuhamia Ubungo, Temeke, Ilala au Kigamboni na kuendelea na biashara hiyo kama kawaida bila kusumbuliwa.

Lakini wakibanwa kila kona, inaweza kuwa rahisi kupambana na biashara hiyo tena kwa mafanikio. Hivyo kilichoanzishwa na Kinondoni, kingefaa kusambaa maeneo mengine ndani ya jiji la Dar es Salaam.

Vilevile, si vibaya kukawa na vita hiyo, katika miji yote ambayo kuna biashara ya madanguro, ili kunusuru mabinti ambayo wamekuwa wakijiingiza huko kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia ya mkato.

Ikumbukwe kuwa, sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zinaruhusu kila Mtanzania kufanya biasshara au kushiriki shughuli yoyote halali ya kumwingizia kipato.

Hivyo, kufanya kazi au biashara halali ni haki ya kikatiba ya kila Mtanzania. Biashara na madanguro sio halali ndio maana inapigwa vita, hivyo, ni vyema wahusika wajue hilo na kuchukua hatua ya kuiacha.

FIKRA MBADALA

# Tume Huru isimamie uchaguzi serikali za mitaa



Pascal Mayalla

KAMA kawaida yangu kila nipatapo fursa, huja na makala zangu elimishi kwa Maslahi ya Taifa ambazo ni kuhusu jambo lolote la kisiasa, kiuchumi au kijamii.

Mnaonaje uhaguzi wa serikali za mitaa ufanyike siku moja na uchaguzi mkuu na usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi? Kama hiyo itafanyika hivyo, Rais Samia Suluhu Hassan atabarikiwa sana.

Mabadiliko haya ya sheria yanaletwa katika mkutano wa bunge hili, hivyo huu ni ushauri kwa Rais Samia na serikali yake katika kubadili sheria ya uchaguzi na kuunda Tume Huru ya Uchaguzi, nashauri tupige ndege wawili kwa jiwe moja? au tuendelee kufanya uchaguzi mkuu na ule wa serikali za mitaa kwa mazoea?

Ndege wa kwanza ni uchaguzi wa serikali za mitaa, usifanyike tena mwaka 2024 wala usisimamiwe tena na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) badala yake ufanyike mwaka 2025 sambamba na uchaguzi mkuu na kusimamiwa na tume huru na shirikishi ya uchaguzi.

Maendeleo ya kweli na maendeleo endelevu ni kukubali kubadilika kwa kwenda na wakati uliopo, tuache kufanya vitu kwa mazoea! Tangu tumeanza kufanya uchaguzi, Tanzania tumekuwa tukifanya chaguzi mbili tofauti kwa muda tofauti, zikitumia sheria mbili tofauti na kusimamiwa na mamlaka mbili tofauti.

Uchaguzi huu ni ule wa serikali za mitaa ambao hufanyika mwaka mmoja kabla ya uchaguzi mkuu na husimamiwa na Tamisemi.

Huku ndiko madudu ya ajabu ya ukiukwaji wa demokrasia huanzia. Chama kinachoshinda serikali za mitaa, ndicho kinachokuja kushinda uchaguzi mkuu unaofuata.

Ukiondoa chama kikubwa na chama kikongwe - Chama Cha Mapinduzi (CCM), vyama vingine vyote vya upinzani Tanzania ni vyama cha mtoto, havioni mbali, hivyo vinajikita kujipanga kwa nguvu kubwa kujiandaa kwa uchaguzi Mkuu wa 2025 kumbe mchezo haswa hufanywa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kwa vile Rais wetu Samia ameonyesha nia njema ya dhati kwa mawazo, maneno na matendo kuwatendea haki Watanzania kwa kukubali kufanya mabadiliko ya sheria ya uchaguzi na kuunda tume huru na shirikishi ya uchaguzi, mnaonaje kama kwenye mabadiliko haya ya sheria yanayokuja, tukapiga ndege wawili kwa jiwe moja?

Kwanza, naendelea kusisitiza kufanya mabadiliko ya sheria bila mabadiliko ya katiba, ni sawa na kula bila kunawa, hivyo tunaipongeza serikali yetu kukubali kubadili sheria ya uchaguzi na kutupatia tume huru ya uchaguzi.

Lakini nashauri tuanze kwanza mabadiliko ya katiba ndipo twende kwenye sheria.

Pendekezo la pili, tufanye uchaguzi wote kwa siku moja na kusimamiwa na tume huru ya uchaguzi.

Kama Zanzibar wanaweza kufanya uchaguzi wa namna tano kwa siku moja , Tanzania hatuwezi kushindwa kufanya uchaguzi wa namna nne kwa siku moja? Yaani ucuaguzi wa serikali za mitaa ufanyike siku moja na uchaguzi mkuu?

Kwa mtazamo wangu, hakuna haja ya kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 halafu uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Kwa sasa tufanye mabadiliko ya katiba na sheria, halafu mwaka 2025 tufanye ucuaguzi mkuu na ule wa serikali za mitaa kwa siku moja. Kwa maeneno mengine, tufanye uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na serikali za mitaa kwa siku moja.

Kwa vile msingi mkuu na matatizo makuu ya uendeshaji wa siasa zetu yako kwenye katiba, katiba ndiyo kichwa cha yote na mengine yote ni kiwiliwili.

Kwa vile kuna mchakato wa katiba mpya utakaanza hivi karibuni, lakini kwa minaajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa wa 2024 na uchaguzi Mkuu wa 2025, tuanze na mabadiliko ya katiba hii hii iliyopo kwa kuibadilisha kwa hati ya dharura, ndipo tuje kwenye mabadiliko ya sheria za uchaguzi na kurekebisha Tume ya Uchaguzi tuunde Tume Huru na Shirikishi ya Uchaguzi.

Kwa maoni yangu, mabadiliko ya sheria bila mabadiliko ya katiba, sawa na kula bila kunawa!. Je, Watanzania tuna haraka sana na uchaguzi hadi tukimbilie kula bila kunawa?

Hitimisho, Kwenye mabadiliko haya ya sheria ya uchaguzi yanayotarajiwa kuwasilishwa bungeni kwa hati ya dharura kwenye mkutano huu, mnaonaje tukimshauri Rais Samia tupige ndege wawili kwa jiwe moja, kwa kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu kwa siku moja au tuendelee na mazoea?

Naamini kabisa Rais Samia ana nia njema kuwatendea haki Watanzania, na Rais msikivu akiongoza serikali yetu ni serikali sikivu.

Pia naomba kutoa angalizo la kitu kinachoitwa karma ambacho viongozi wetu hawakijui na matokeo ya kuidharau karma.

**Wasalaam.**
**Paskali**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Viongozi Afrika fikirieni pia watu wenu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Ni kawaida kuwa Rais hakuwa na jukumu la kujua nini kinanunuliwa kwa ajili ya Ikulu na kwa gharama gani bali ni kupokea na kutumia bila maswali. Lakini tunajuana, huyu akaona isiwe shida, akahoji kwani ni kodi ya wananchi ndiyo inatumika?**

WAHENGA wetu enzi zao walipoangalia maisha yalivyokwenda huku yakigubikwa na vurugu, inda, uonevu, dhuluma na chuki, wakaja na semi mbalimbali za kusaidia kuweka mambo sawa.

Tulipokua tukakuta semi kama 'ukishangaa ya Musa utayaona ya Firauni', 'aliye nacho huongezwa na asiye nacho hunyang'anywa hata kidogo alicho nacho', pia 'usipoziba ufa utajenga ukuta' na 'asiyesikia la mkuu huvunjika guu'.

Hizo ni sehemu ndogo tu ya semi zilizotumika kuweka mambo sawa katika familia na jamii kwa ujumla ingawa ziko ambazo zimepitwa na wakati. Hata hivyo, ziko zinazoendelea kutumika kwa nia njema ya kuelimisha na kuonya.

Usemi wa 'aliye nacho huongezewa na asiye nacho hunyang'anywa hata kidogo alicho nacho', hivi sasa unaonekana kutamalaki sana Afrika na unatumika kuonyesha jinsi wanyonge wanavyoonewa, huku wenye nguvu wakitamba.

Kuna kiongozi fulani katika Afrika ambaye yuko madarakani, hivi karibuni aliamua kwenda tofauti na usemi huo baada tu ya kuchaguliwa kuongoza nchi hiyo, alistaajabisha hata waliomchagua kuingia Ikulu.

Mara tu baada ya uchaguzi na kutangazwa mshindi, kabla hata hajaapishwa kukalia kiti, wasaidizi wake haraka sana walimfuata na kumwomba atie saini makaratasi waliyompelekea.

Katika kutaka kujiridhisha ili asiuziwe mbuzi kwenye gunia, kiongozi huyo akaomba ayasome kwanza. Alipopitia mistari akaonekana kushangazwa na maudhui na kuhoji wale wasaidizi kana kwamba hakuelewa.

Akataka kujua anatia saini ili iweje! Wasaidizi nao wakaonyesha kumshangaa kwa sababu ilikuwa kawaida kwamba kiongozi kama yeye akishaingia madarakani, basi alitakiwa kununuliwa magari mapya sambamba na mahitaji mengine.

Kilichomshangaza ni kununuliwa magari na si gari. Kabla hajauliza, wale wasaidizi wakamwambia "Mheshimiwa, ni kawaida Rais akishaingia madarakani, apate vifaa vipya vya kutendea kazi, yakiwamo magari mapya."

Aliwatazama na kuwauliza: "Kwani yaliyokuwa yakitumika awali na mtangulizi wangu yamekwenda wapi? Yameharibika? Yameuzwa? Yamehamishwa?" Akajibiwa: "Hapana Mheshimwa yapo." Akasema: "Kama ndivyo nitatumia hayo hayo."

Hakutaka kutumia fedha za umma kununulia magari mengine, wakati yaliyokuwapo bado yalikuwa yanafaa kutumiwa na mtu mwenye nafasi kama yeye. Wasaidizi waliondoka vichwa chini, kwa sababu mpango wao wa upigaji uligonga mwamba.

Ni kawaida kuwa Rais hakuwa na jukumu la kujua nini kinanunuliwa kwa ajili ya Ikulu na kwa gharama gani bali ni kupokea na kutumia bila maswali. Lakini tunajuana, huyu akaona isiwe shida, akahoji kwani ni kodi ya wananchi ndiyo inatumika?

Alijua kama watu wake wangepata shida wangemlilia yeye kwani ndiye mwenye jukumu na wajibu wa kuhakikisha shida hazipo na wanaishi maisha ya raha na maendeleo bila matatizo wala kadhia yoyote.

Nakumbuka siku moja, Rais Julius Nyerere alisema kila alipopita mitaani na kuona maskini wakiombaomba na wamesawajika kimaisha, alijua tu kuwa ule ulikuwa mzigo wake. Sina uhakika kama viongozi wa leo nao wana hisia kama hizo.

Sina uhakika pia na idadi ya viongozi Waafrika wenye hisia kama za kiongozi huyu aliyekataa magari mapya lakini pia Nyerere aliyeguswa na maisha ya watu wake walio mitaani wakiteseka na umasikini.

Wakati mambo yako hivyo, tumethibitishiwa pia kupitishwa kwa Muswada wa Mafao kwa Wenza wa Viongozi wa nchi hii, uliopitishwa kwa bashasha na Bunge letu hivi karibuni.

Kwamba endapo itakuwa sheria baada ya kutiwa saini na Rais, basi kama wewe ni mke, mume, mjane au mgane wa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu awe mstaafu au madarakani, na wengine wa ngazi hizo, sasa usiwe na shaka kabisa, mambo ni bulbul!

Yaani kama wewe ni wa familia hizi, ah pepo inakushukia duniani sasa hivi, huku wenzio wanaotoka familia za pangu pakavu tia mchuzi, familia za kajamba nani, familia za kauka nikuvae, wakitesekea maisha.

Hivi kweli kulikuwa na haja sana ya kufanya haya katika nchi hii masikini kweli? Hizo fedha za kodi za wananchi kwa nini wasingepewa vijana waliomaliza shule na vyuo na kuranda mitaani kutafuta kazi wakajiajiri?

Nchi hii kweli hivi sasa haina matatizo ya wananchi kwenye maji, umeme, tiba, chakula na mengineyo, kiasi cha kuacha kupeleka huko fedha hizo na badala yake kupeana hivi hivi, tena wengine wanaotarajiwa kuzipata wakiwa na kazi za kuwaingizia kipato?

Waheshimiwa sana wabunge kama mnavyopenda kuitwa, chonde chonde, hili mngelifikiria sana kabla ya kulipitisha, hata kama ninyi mna mishahara na marupurupu chekwa, kuna watu huku mitaani mlo mmoja ni kwa mbinde. Sijui na sina uhakika mtawaeleza nini waelewe kwenye kampeni zenu.

**Mungu na atusaidie!**

# Matinyi ataka viongozi kueleza yanayofanyika

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Idara ya Habari MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, amesema viongozi wa serikali wanatakiwa kuwaeleza wananchi miradi iliyotekelezwa kuondoa pengo kati ya wanachokiona na kinachofanywa.

Amesema ni jukumu la viongozi na watendaji kueleza wanachi makubwa yanayofanywa na serikali kupitia mikutano mbalimbali.

Akizungumza katika mkutano wake jana uliofanyika mjini Kibaha, mkoani Pwani na kuhusisha viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa huo, Abubakar Kunenge, serikali inapeleka fedha nyingi za miradi ya maendeleo kwa maslahi ya wananchi.

Alicha licha ya serikali kufanya hivyo, wananchi hawaelezwi michanganuo na mengine ambayo yamefanyika.

Alisistiza kuwa viongozi wa mikoa wanatakiwa kusimamia fedha za utekelezaji wa miradi hiyo ili iweze kuleta matokeo chanya kwa wananchi sambamba na kuwashirikisha kwa kila hatua kwenye maeneo husika.

Kuhusu mkutano huo, Matinyi alisema ni moja ya mpango uliozinduliwa hivi karibuni jijini Dodoma kuelezea utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyofanywa na serikaii kwa kipindi cha miaka mitatu na itahusisha mikoa yote 26 ili taarifa ziwafikie wananchi.

Kunenge alisema katika kipindi cha miaka mitatu mkoa huo umepokea Sh. trilioni 1.19 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi ya afya, elimu, maji na miundombinu na hivyo kupunguza vikwazo vilivyokuwa vinawakwamisha maendeleo kwa wananchi.


Kuhusu miradi ya miundombinu ya barabara, kiongozi huyo alisema serikali ipo mbioni kuanza ujenzi wa upanuzi wa barabara kuanzia Dar es Salaam, Chalinze na Morogoro ambayo itakwenda kuondoa msongamano.

Pia alisema ujenzi wa barabara ya Chalinze-Utete itafungua milango ya kiuchumi na maendeleo katika maeneo hayo.

Katika mkutano huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Hemed Magaro, aliishukuru serikali kwa namna ilivyotoa fedha za miradi ambayo imekwenda kutatua vikwazo kwa wananchi hususani katika eneo la delta.

Magaro alisema awali wananchi wa Mbwera awali walikuwa wanasafiri kilometa 90 kwenda kupata huduma za afya na wakati wa mvua walikuwa hawawezi kusafiri, hivyo ujenzi wa kituo cha afya katika eneo lao umeondoa tatizo lililokuwa linawakabili.

Alisema ongezeko la vituo vya afya pamoja na vifaa tiba katika Halmashauri hiyo, imechangia kupunguza vifo vya mama na mtoto.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), CPA Hosea Kashimba, kabla ya mazungumzo yao katika ofisi yake iliyopo kwenye ofisi za Bunge, jijini Dodoma, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Hospitali kuchunguza magonjwa ya moyo bure

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya DSB iliyoko Upanga jijini Dar es Salaam leo inaanza kambi ya siku mbili kwa ajili ya uchunguzi wa matibabu ya moyo bure kwa watoto na watu wazima.

Akizungumza na gazeti hili jana, daktari wa hospitali hiyo, Isa Mbashu alisema wamekuwa wakiandaa kambi kama hiyo kila mwaka kwa ajili ya kuadhimisha siku ya ugonjwa wa kiharusi.

Alisema wataendesha kambi hiyo kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka taasisi ya Heart Foundation na kuwataka wananchi kutumia fursa hiyo kufanya uchunguzi wa afya ya moyo.

Alisema siku ya kiharusi huadhimishwa kila tarehe 29 ya Oktoba kila mwaka na kwamba ugonjwa huo umekuwa ukisababishwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama sukari na shinikizo la damu.

Alisema wameamua kuweka kambi hiyo ili kuwapima watu viashiria vya ugonjwa huo ili wapate tiba mapema wanapogunduliwa kuwa na matatizo badala ya kusubiri hali kuwa mbaya.

"Watakaokuja hapa watapimwa shinikizo la damu ambalo pia ni kisababishi kikuu cha ugonjwa wa kiharusi, watapimwa sukari ambayo nayo huwa inatajwa kusababisha kiharusi na magonjwa haya mara nyingi yagunduliki mapema mpaka hali inapoanza kuwa mbaya," alisema

Alisema watapima kujua kiwango cha umeme wa moyo ECG, oksijeni iliyoko mwilini na namna moyo unavyofanyakazi kwaajili ya kuangalia chemba na valvu za moyo, mishipa ya damu kwenye moyo pamoja na viashiria hatarishi vya magonjwa yote.

Alisema wananchi watakaojitokeza kwenye kambi hiyo watapata ushauri kutoka kwa madaktari bingwa kuhusu hatua za kuchukua kujiepuesha na maradhi mbalimbali yanayoambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Alisema mbali na ushauri wa afya, wananchi watakaofika watapata ushauri kuhusu lishe bora ili kujiepusha na maradhi mbalimbali na watakaokutwa na matatizo watashauriwa pia kuhusu dawa ambazo wanaweza kutumia.

"Tuna kipimo cha moyo ambacho huwa wagonjwa wengi wanashindwa kupata vipimo vyake kutokana na gharama kubwa kinaitwa Stress ECG, unakuta mgonjwa anamaumivu ya moyo lakini kila akipimwa hakuna kinachoonekana lakini akipimwa kwenye hiki kipimo kila kitu kitaonekana," alisema.

# Chuo Kikuu Butiama chaanza kudahili wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MJNUAT

Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT) kimeanza kufanya udahili wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2023/24. Kazi hiyo ilianza Oktoba 13, 2023 baada ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kukiruhusu chuo hicho kufungua dirisha la udahili ambalo linatarajiwa kufungwa Novemba 14, 2023.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Lesakiti Mellau, alithibitisha juzi kuwa kuwa chuo hicho kimefunguliwa dirisha la kudahili wanafunzi na TCU.

"Tumeshafunguliwa dirisha la waombaji kwa wanafunzi watarajiwa. dirisha lilifunguliwa pamoja na vyuo vingine (dirisha la nne) na chuo kimeongezewa muda wa dirisha kuwa wazi hadi Novemba 14, 2023 ili wanafunzi wengi waombe kujiunga na chuo chetu," alisema Prof. Mellau.

Prof. Mellau alisema chuo hicho kinatarajia kudahili wanafunzi wasiozidi 150 katika programu tatu za Shahada ya Sayansi ya Kompyuta, Sayansi katika Kilimo Uchumi na Kilimo Biashara, na Shahada ya Sayansi katika Elimu ya Viumbe Hai vya Majini.

"Tumeamua kuchukua wanafunzi 150 kwa sababu kwanza idadi hiyo ni nzuri kwa mwalimu kufundisha kivitendo na pili tumeamua kuchukua wanafunzi 150 kutokana na nafasi ya kulala wanafunzi kulingana na miundombinu iliyopo," alisema.

Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia kimeanza kufanya udahili wa wanafunzi kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015 baada serikali kutoa Sh. billion 2.661 kwa ajili ya kukarabati Kampasi ya Oswald Mang'ombe mwishoni mwa mwaka wa fedha 2022/23.

# MAISHA

NOVEMBA 5, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 14




## Juisi ya Pera

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15






## KATUNIKA


Ukurasa 16





# MITANDIO INANOGESHA UREMBO WA KICHWA

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ■ | T | A | N | G | A |
| I | ■ | ■ | ■ | U | ■ | S |
| N | ■ | T | I | N | ■ | I |
| G | O | A | ■ | D | O | M |
| I | ■ | N | O | A | ■ | I |
| D | ■ | D | ■ | ■ | ■ | K |
| A | F | U | T | E | ■ | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MIA, ARS, RAI, HAO, APETE, CHIZI, AOMBE, IMARA, INGIZWA, TAAHIRA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Watoto wawili walikuwa wakigombea mapera, mama mmoja alitokea na kuwaamulia na kuwataka kila mmoja kusema tatizo ambalo limewafanya kugombana.

Juma: John ndiye mgomvi alinipora mapera yangu

John: Hapana yeye ndiye mgomvi alichukua mapera katika mti aliopanda baba

Juma: Ule mti umejiotea pale msituni, huyu ni muongo

Mama: Nyinyi wote nawaona mnadanganya ugomvi haufai kwa sababu huleta chuki

John: Kweli mama hata mwalimu alisema heri nusu shari, kuliko shari kamili

**SWALI**

Je sukari inayotumika nyumbani inatengenezwa kutokana na zao gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Asili zetu chanzo kikubwa cha matatizo yetu!

KARIBU msomaji wangu. Wiki iliyopita mada ilikuwa kwa nini pombe inaua hatima ya vijana wengi. Nilijaribu kueleza kidogo athari za pombe kiafya, kwa mujibu wa wataalamu wa afya.

Lakini pia yatupasa kutambua kuwa matatizo mengi yanayowatesa watu, ukiwamo ulevi wa kupindukia hayakuanza leo. Yalishakuwepo tokea zamani!

Kabla sijaendelea hebu msomaji wangu, nikupe maoni ya msomaji wetu kuhusu makala ya wiki iliyopita. Anasema: "Hiyo kiukweli inaumiza. Nimepata stori ya huyo kijana ambaye anatumia pombe kupita kiasi. Hilo si pepo wala mapepo.

"Hayo ni mazoea aliyojizoesha, mwili ukitawaliwa hushindwa kujidhibiti. Nashauri asaidiwe kijana wa namna hiyo kwani hata kwenye familia yetu yupo. Hivyo ndugu wakazane tu japo ni kazi ngumu.(Timo Kilagusi wa Iringa)".

Mpenzi msomaji, bila shaka umempata msomaji wetu huyu. Naye anakiri kuwa katika familia yake yupo kijana anayeteswa na unywaji wa pombe kupita kiasi. Na inavyoonekana hata wao wamekata tamaa kwani anakiri ni kazi ngumu.

Katika kupitia maandiko ya Mungu, nimegundua iko siri kubwa sana kuhusu maisha ya wanadamu. Hakuna kitu kinachotokea ambacho hakikuwepo kabla na jinsi ya kushughulika nacho pale mambo yanapokwenda mrama.

Mungu anasema katika moja ya maandiko yake kwamba; Yaliyokuwako ndiyo yatakayokuwako; na yaliyotendeka ndiyo yatakayotendeka; wala jambo jipya hakuna chini ya jua.

Je! Kuna jambo lolote ambalo watu husema juu yake. Tazama, ni jambo jipya? Limekwisha kuwako, tangu zamani za kale zilizokuwa kabla ya sisi. Hakuna kumbukumbu lolote la vizazi vitakavyokuja, miongoni mwao wale watakaofuata baadaye.

Mahali pengine neno la Mungu linasema;- Yale yaliyoko yamekuwako na hayo yatakayokuwako yamekwisha kuwako; naye Mungu huyatafuta tena mambo yale yaliyopita.

Msomaji wangu, hapo tunaambiwa kuwa kinachotokea sasa katika maisha yetu siyo kipya kwani kilishakuwako huko kabla. Hii inamaanisha kwamba, matatizo yanayotupata hivi sasa yalishakuwako! Yalifanywa pia na mababu, mabibi zetu na hata wazazi.

Mfano, kabla ukoo au familia fulani katika miaka hiyo ya zamani walikuwa walevi, walikuwa wazinzi, walikuwa wacha Mungu....na kadhalika, kwanini asili hiyo isijidhihirishe leo hii katika maisha tunayoishi? Upo uhusiano mkubwa sana wa maisha tunayoishi na yale ya zama za kale.

Mila na desturi zetu zina uhusiano mkubwa sana na mizimu. Yawezekana mtu alitolewa sadaka na wazazi wake pasipo yeye kujua. Au yeye mwenyewe alijitoa sadaka kwa mizimu kwa kujua ni sahihi kumbe ni maangamizi. Sasa anapokumbwa na matatizo yanayoshindikana anafikiri kuwa amelogwa kumbe asili yake ndiyo chanzo.

Kama mababu, mabibi na hata wazazi wetu wa sasa bado wanaabudu mizimu/matambiko, lazima vizazi vyetu vya sasa pia vitaunganishwa nayo. Wazazi pamoja na nguvu/karama kubwa waliyopewa na Mungu, lakini wamechangia sana mateso, mikosi na balaa zinazowapata watoto wao.

Hebu angalia, Neno la Mungu linasema; Naam, walitoa wana wao(wavulana) na binti zao, Kuwa dhabihu kwa mashetani. Wakamwaga damu isiyo na hatia, Damu ya wana wao na binti zao, Waliowatoa dhabihu kwa sanamu za Kaanani; Nchi ikatiwa unajisi kwa damu. (Kaanani nchi ya wapagani- wasio na dini).

Leo hii wapo baadhi ya wazazi ambao waliwapeleka watoto wao wenyewe kwa waganga wa kienyeji, wakachanjwa chale pasipo kujua kuwa huko ni kuwakabidhi mashetani wamiliki maisha ya watoto wao kama andiko hilo hapo juu linavyothibitisha.

Mzazi mwenyewe akimpeleka mwanae kwa mganga, basi shetani anayo haki na mtoto huyo kumfanyia vile atakavyo.

Mfano, baba anamkataa mtoto akiwa tumboni mwa mamaye kuwa si wake, mtoto huyu akija kukataliwa na jamii atamlaumu nani? Oh! Sitaki mtoto wa kike, mama anazaa wa kiume, lakini mtoto huu akikua anaanza kusuka nywele, kuvaa heni, au anakuwa na tabia za kike huku marafiki zake wakiwa wa kike tu. Je, kwa hili utamlaumu nani? Kumbe ni yale maneno yako uliyotamka.

Kumbuka maneno huumba. Hata Mungu alitamka na vyote vikatokea. Kwanini nawe ukitamka lisitokee? Ulimi wako waweza kuwa sumu kwako na familia yako. Na yanayotokea leo yalishakuweko kabla, tusishangae sana. Unachotengeneza leo, utakikuta mbele ya safari, kiwe kizuri au kibaya. Maisha yana tabia ya kujirudia!

***Kwa maoni tuma kupitia namba 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kuita wakwe 'malboro nyeusi' ni kuwakosea

IMENIUMA sana. Haipendezi na inasikitisha kusikia kuna aina mpya ya ukatili imeingia mjini ya kuwaita mama mkwe, malboro nyeusi.

Unajua kwa nini wanawaita wakwe zao jina hilo baya? Eti wana kelele nyingi, wanafiki na ni watu wanoko.

Wanawachukulia kwamba ni watu wenye gubu. Sababu za msingi za kufanya hivyo ni nini? Eti kwa nini wako karibu zaidi na watoto wao wa kiume. Hivi hujui kuna vinasaba hivyo kati ya mtoto wa kiume na mama yake?

Ninyi wanawake wa kisasa, enyi wanaume wa kisasa, mnawakosea sana wazazi wenu. Mama wa mumeo ni mama yako, na baba wa mkeo ni baba yako.

Kwa nini hamwoni aibu mkaacha kuwadhihaki? Kila kukicha wewe maneno hayakukosi, huyo mama huyo, halafu hako kababa hako unavyokaona, hakana koromeo (akimaanisha sauti) kamekaliwa na huyo mama.

Maneno gani hayo kwa wazazi? hivi akiwa mama yako kaitwa malboro nyeusi itakufurahisha? unasahau na wewe ni mkwe mtarajiwa?

Ukisikia tu simu imepokelewa, mumeo kasema mama unaendeleaje? Nimekumisi mama yangu, unavuta mdomo, hasira kibao na chakula unaharibu jikoni.

Hata ikitokea mama yake mzazi akapiga simu kumjulia hali mwanae au kumueleza hali yake au ya baba yake sio nzuri kiafya, mgogoro unaanza.

Unataka mama amuambie nani kuhusu afya yake? au afya ya baba yake? Kati ya wewe na mama mkwe nani hapo ana gubu?

Nyie wadada nyie, Mungu anawaona. Tengenezeni mambo yenu mapema. Chawa wanasubiri kutangaza na kuusambaza ubaya wako tu.

Mazuri yako uliyoyafanya wakaona kwa macho yao, hawataki kuyazungumza. Ni ubaya ubaya tu.

Hata kama mama mkwe ni mbaya kiasi gani, sio sababu ya kumdhihaki na kumuona hana thamani. Si kwa sababu wakwe, hawapaswi kuingilia ndoa ya watoto wao ambao ni watu wazima.

Imagine huyo ni mama yako na umesikia akiitwa hivyo na wifi yako. Kitakachojiri katika moyo wako, fikra zako ni Mungu pekee anayejua. Ikikuuma acha kudhalilisha wazazi wa mwenzio. Mzazi wako ni mzazi wake.

Hata kama tabia, fikra na mienendo yetu haiwezi kubadilika kwa siku moja, piga moyo konde, waheshimu na waone ni wazazi wako.

Hapo utayaona maelewano ndani ya nyumba yako.Mume anaweza akanyamaza lakini moyoni hauna nafasi tena kwa sababu ya kuwadhalilisha wazazi wake.

**"Ninyi wanawake wa kisasa, enyi wanaume wa kisasa, mnawakosea sana wazazi wenu. Mama wa mumeo ni mama yako, na baba wa mkeo ni baba yako.**

Yangu ni hayo. Shukrani zangu ni kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, ambaye ameonekana akiunga mkono uamuzi wa wananchi kutunga sheria ndogo inayolenga kuzuia mmomonyoko wa maadili ni hatua kubwa kwa jamii yetu, kubeba ajenda za kusaidia jamii kwenda mbele hasa katika maadili, fursa za kiuchumi na kupinga ukatili.

Dk. Gwajima anasema jitihada hizo za kukabiliana na mmonyoko wa maadili ni kudhibiti mmonyoko huo kwenye jamii.

Wananchi wenyewe, kumiliki ajenda ya kupambana na mmonyoko wa maadili, ni mfano wa jkuigwa na kila mtu.

***•Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.***

***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com***


***Simu ya mkononi: +255 767 535490***

# HARUSI





Kama unatarajia kufunga harusi na hujui gauni gani litamkaa vyema bi harusi? Basi magauni haya yenye asili ya India yanafaa zaidi.





# MITINDO



## MITANDIO INANOGESHA
### urembo wa kichwa

UNAWEZA kuongeza nakshi ya mavazi kwa kufunga kitambaa cha mtandio kichwani ili kukupa mwonekano wa kuvutia.

Kitambaa hiki cha kichwani kinafungwa katika mitindo mbalimbali ambayo inaongeza ubunifu na umaridadi wa mtu husika.

Pengine vazi hili ni jibu kwa wanawake wengi ambao wanaumiza vichwa kuhusu watoke vipi pale wanapotaka kwenda kwenye mialiko au kazini.

Mara nyingi wanawake aina ya nywele zinakuamulia uvae vazi gani, lakini mtandio wa kichwani unakuondolea chaguo na kukupa uhuru wa kufanya vyovyote unavyohitaji.

Kwa wale ambao wamesuka nywele muda mrefu mtandio utakufanya kuonekana na taswira mpya.


Unaweza kufunga kitambaa chako kulingana na rangi ya kiatu au vazi ulilopigilia na ukabadili kila siku.

Mtandio unaweza kufunga hata kwenye nywele fupi au ndefu inategemea tu na mpangilio wako.

Mara nyingi hufungwa kwa kitambaa kilichokunjwa kwa mfumo wa pande nne kuacha pembe mbili ndefu au unakikunja mara nne zaidi.

Aidha, kuna mitandio ambayo tayari ipo katika mfumo wa ubunifu hivyo kazi yako ni kufunga tu.







UREMBO

Na Mary Geofrey

# Mng'ao wa kucha za asili

WANAWAKE wengi wanapenda kuweka kucha kuwa safi kwa kupaka rangi na hina wakati wote.

Hata hivyo, kuna wale ambao hawapaki chochote na wanataka kucha zao kuwa safi na nyeupe,

Loweka kwa maji vuguvugu

Wakati unahitaji kucha zako kuwa za kung'aa unahitaji mara kwa mara kuloweka vidole vyako katika maji vuguvugu.

Hii ni kwasababu maji vuguvugu husaidia kuboresha kucha na kuondosha rangi za kucha.

Tumia sabuni ya asili na scrub ya kucha kusafisha.

**Sugua na limao**

Kama wewe ni mpenzi wa kupaka rangi za kucha mara kwa mara basi ni lazima utakua na kucha za njano, ili kuweza kuwa ang'avu jaribu kusugua kucha zako na kipande cha limao mara kwa mara.

Unaweza pia kutengeneza dawa hii nyumbani changanya kijiko kimoja cha baking soda, kijiko cha limao na kijiko kimoja cha mafuta ya mzaituni kisha changanya vizuri na sugua katika kucha zako na ukimaliza osha kwa maji safi. Hii itazipa kucha zako afya,ung'aavu na nguvu.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# JUISI YA PERA

MAPERA ni matunda yanayopatikana kwa wingi lakini mara nyingi huwa watu hawayapendi kutokana na kuwa ni tunda gumu na kuleta bughudha wakati wa kutafuna.

Hata hivyo matunda haya yana faida kubwa kwa afya ya mwanadamu.

**Mahitaji**

Mahitaji ni mapera matano, pasheni tisa, sukari kiasi, maji kiasi.

Namna ya kuandaa

Osha na katakata mapera kisha tia katika mashine ya kusagia (blender) na usage kwa maji kiasi kisha yachuje.

Kata pasheni toa nyama yake kisha saga katika blender kwa maji kiasi .

Changanya pamoja na juisi ya mapera na tia sukari kiasi kadiri upendavyo ikiwa tayari

**Faida zake**

**Vitamin C**

Mapera yana utajiri wa Vitamin C ambayo ni muhimu katika mwili wa binadamu.

**Kinga ya kisukari**

Ulaji wa watu wengi unawaweka katika hatari ya kupatwa na ugonjwa wa kisukari lakini matumizi ya mapera yatakupunguzia hatari ya kupatwa na ugonjwa wa kisukari Hii ni kwa sababu mapera yana utajiri mkubwa sana wa Fibre.

Fibre ni muhimu sana katika kupunguza kiasi cha sukari kwenye damu. Vilevile ni muhimu sana katika kuusafisha mfumo kwa usahihi.

**Kuimarisha kuona**

Mapera yana utajiri wa Vitamin A au Retinol ambayo ni muhimu katika kusaidia kuona vizuri.

Hivyo basi kama ilivyo kwa karoti, mapera yanasaidia katika kuongeza na kuimarisha uwezo wa mtu kuona.

Kusaidia katika Uzazi

Mapera yana madini yaitwayo Folate ambayo husaidia katika kurutubisha mayai ya uzazi.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# MASIKA NDIO WAKATI MWAFAKA WA KUTAFUTA NYUMBA SAHIHI YA KUISHI

MSIMU wa mvua umewadia, kipindi ambacho ni muhimu katika kutafuta makazi kwa ajili ya kuishi au viwanja vya kujenga nyumba.

Hiki ndicho kipindi ambacho kinamsaidia mtafutaji wa nyumba ya kuishi au mwenye malengo ya kujenga nyumba kupata sehemu sahihi ambayo haiko katika eneo linalojaa maji.

Si rahisi kutambua eneo linalojaa maji unapofanya uamuzi wa haraka wa kununua, kupanga au kujenga nyumba katika kipindi cha kiangazi ndiyo maana wale wanaofanya hivyo wakati mwingine huingia kwenye majuto au hasara pale wanapojikuta kuzingirwa na maji inapofikia masika.

Kwa kuwa tayari kipindi cha masika kimefika na mvua za kutosha zinanyesha, ni wakati mwafaka watafutaji wa nyumba au viwanja kukitumia kwa ufasaha ili baadaye wasiingie kwenye majuto.

Wataalamu katika sekta hii ya ujenzi wanashauri kwamba katika utafutaji wa nyumba ya kuishi hususani kwa wanaopanga yapo baadhi ya mambo muhimu ambayo mtu akizingatia hawezi kupata msongo wa mawazo ambao umekuwa ukiwakuta wengi wanaopanga bila kuzingatia hayo.

Miongoni mwa mambo hayo yanayotajwa na wataalamu ni pamoja na kuwa makini na nyumba iliyopo kwenye eneo la bonde na umbali hata kama muonekano wake unavutia kiasi gani.

Kwamba kuna uwezekano mkubwa mtu akavutiwa na mwonekano mzuri wa nyumba na akaamua kupanga au kununua kwa ajili ya kuishi lakini baadae ikamsababishia majanga baada ya kunyesha mvua kubwa.

Kadhalika, wanashauri kwamba nyumba iliyo mbali zaidi inayomlazimu mtu kutumia gharama kubwa anapokwenda kwenye shughuli zake na kurejea, nayo si nzuri sana labda kama anaimiliki mwenyewe hususani katika nyakati hizi za mvua.

Endapo unatumia usafiri wa umma na inakulazimu kila ukifika kituoni ni lazima utumie tena usafiri mwingine ambao nao ni gharama kubwa kufika kwenye nyumba hiyo ni lazima ufikirie kwa makini kufikia uamuzi wa kuishi kwenye nyumba hiyo. La sivyo unaweza kushindwa kuweka akiba kwa ajili ya kufanyia maendeleo mengine au mvua zinaponyesha kwa wingi ikakupa taabu sana kutoka au kurejea.

Jambo lingine la muhimu la kuangalia kabla ya kupanga nyumbaambalo wanashauri ni kama inavuja na kwamba hili linaweza kutokea kwa nyumba zilizo bondeni au zisizo bondeni.

Kuna baadhi ya nyumba zinakuwa zinaonekana vizuri kwa nje, lakini ndani zinakuwa zinavuja na hivyo wakati mwingine kuhitaji marekebisho makubwa ambayo huenda yakakuongezea gharama kubwa ambazo hukutegemea, kwa hiyo inabidi ujiulize kama kuna ulazima wa kuishi kwenye nyumba hiyo au kama unaweza kutafuta nyingine na ukaepuka hayo isipokuwa tu kama mmiliki yuko tayari kurekebisha kwa gharama zake mwenyewe.

# Panga stoo ufukuze mende, panya

**Na Restuta James**

LEO tuangazie chumba chetu cha kuhifadhia vitu, stoo zetu za jikoni. Chumba hiki kisipotunzwa vizuri kinageuka kuwa kichaka cha mende, panya na wadudu wengine.

Niseme tu kwamba mpangilio na usafi utaiweka stoo yako kwenye kiwango kizuri mwaka mzima hata kama hauna shelf au makabati.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa watu wengi wanajisahau kwa upande wa stoo za jikoni jambo linalosababisha isiwe sehemu nzuri ya kuhifadhi vitu na hususani vyakula badala yake panakuwa 'jalala' la ndani.

Wanaeleza kuwa stoo zilizogeuka jalala hazina mpangilio na hivyo baadhi ya vitu vinasahaulika.

"Mpangilio ni kiini cha usafi ndani ya nyumba na hasa stoo. Utakapoweza kupangilia utakuwa umejikomboa jumla," anasema Joyce Boaz.

"Unatakiwa kuweka vyakula kwenye makopo yanayoonyesha ndani, kama ni ya kioo au plastiki, kama huna aina hiyo weka lebo ili utakapotaka kutumia iwe ni rahisi kujua nini uchukue na urudishe kiurahisi," anafafanua.

Anasema stoo ni sehemu ambayo vitu vyote vinapaswa kuonekana "siyo sehemu ya kutafuta vitu."


Anashauri kuwa vitu vizito kama ndoo za nafaka vinatakiwa viwekwe shelf za chini na vyepesi kama viungo vikae juu.

Joyce anasema vyombo visivyotumika mara kwa mara vifungwe vizuri ili kuzuia kuharibika.

Anasema katika mpangilio, vyakula visiwekwe pamoja na vifaa vingine kama sabuni..



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...MAISHA KAMA KIOO UKIYACHEKEA YANAKUCHEKEA

RIPOTI MAALUM

# SIRI NZITO GAZA

## -Wakazi wake kuhamishwa baada ya vita?

**Na Mwandishi Wetu**



MAPIGANO yanaendelea katika Ukanda wa Gazi, yanazidi kuleta hofu hatma ya eneo hilo baada ya vikosi vya Israel kuendelea kushambulia kupitia anga, majini na ardhini.

Mpaka sasa kwa mujibu wa serikali ya Hamas ambayo inatawala ukanda huo, watu zaidi ya 9000 wamepoteza maisha na nyumba nyingi kuporomoshwa chini.

Katika vita hiyo Waisrael zaidi ya 1500 wameuawa baada ya wanamgambo wa Hamas kufanikiwa kuingia ndani ya Israel na kufanya shambuzi la kushtukiza Oktoba 7, mwaka huu.

Tangu kufanyika shambulio hilo, Israel imeapa kuliangamiza Hamas, imetangaza kusambaratisha Gaza kwa kile wanachokiita mapigano ya haki dhidi ya watu wake.

Umoja wa Mataifa umetoa kauli kuhusu kuzingirwa Gaza na majeshi ya Israel, ikionya ndani ya eneo hilo hakuna maisha bali sawa na janga la kibinadamu.

Wanajeshi wa Israel wamelizingira eneo lote la Gaza na kuzuia kitu chochote kuingia wala kutoka na kusababisha watu kukosa chakula, maji, umeme na mafuta.

Eneo lote la Gaza linakaliwa na watu milioni 2.4 ambao ni Wapalestina na wafanyakazi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Mzozo una miaka 100

Mzozo wa Waisrael na Wapalestina umedumu zaidi ya miaka 100, tangu Uingereza ilipochukua udhibiti eneo hilo baada ya utawala wa Ottoman kushindwa katika vita vya kwanza vya dunia.

Wakati huo ardhi hiyo ilikuwa ikimilikiwa na Wayahudi walio wachache na Waarabu walio wengi.

Uhasama baina ya makundi hayo mawili ulianza wakati jamii ya kimataifa ilipoipatia Uingereza jukumu la kuwapatia makazi Wayahudi katika eneo la Wapalestina.

Kwa upande wa Wayahudi eneo hilo wanaliona kama urithi kutoka kwa mababu zao, lakini Wapalestina ambao ni Waarabu nao wanaona wana haki ya kumiliki tangu enzi.

Kati ya mwaka 1920 hadi 40, Idadi ya Wayahudi katika eneo hilo iliongezeka, wengi wakikimbia kuwa barani Ulaya na hasa baada ya mauaji ya Holocaust yaliyofanywa na Adolf Hitler katika vita ya pili ya Dunia.

Mwaka 1947, Umoja wa Mataifa ulipiga kura kugawanya eneo la Palestina na kuwa mataifa mawili ya Israel na Palestina na mji wa Jerusalem ukiwa wa kimataifa.

Mpango huo ulikubaliwa na Wayahudi lakini Wapalestina waliukataa.

**TAIFA LA ISRAELI**

Mnamo 1984 ,baada ya kushindwa kutatua mzozo huo, watawala wa Uingereza waliondoka na viongozi wa Kiyahudi wakatangaza uanzishwaji wa taifa la Israel.

Wapalestina wengi walipinga na vita vikaanza na kujumuisha mataifa jirani ya Kiarabu kuvamia eneo hilo.

Jordan iliteka aradhi iliyojulikana baadaye kama Ukingo wa Magharibi, huku Misri ikilinyakua eneo la Ukanda wa Gaza.

Jerusalem iligawanywa kati ya wanajeshi wa Israel waliopo magharibi na wanajeshi wa Jordan waliopo mashariki.

Kwa kuwa hakukuwepo kwa mkataba wa amani - kila upande ulilaumu mwengine kuibua zaidi kwa miongo kadhaa.

**NDANI YA PALESTINA**

Palestina ina vyama viwili vyenye nguvu Hamas na Fatah.

Kwa muda mrefu, chama cha Fatah ambacho kiliasisiwa na Yasser Arafat, kiliongoza Mamlaka ya Palestina chini ya Israel.

Uchaguzi wa Bunge wa mwaka 2006 uliingiza Palestina kwenye machafuko ya wenyewe kwa wenyewe baada ya Hamas kushinda viti 74 vya ubunge na Fatah walipata viti 45. Vyama vingine viliambulia viti 13.

Fatah waligomea matokeo hayo na hapo yakaibuka mapigano baina ya Hamas na Fatah.

Hamas waliunda Serikali ambayo ilisusiwa na Fatah. Serikali ya Hamas ilikumbwa na kibano kikali kutoka Israel, Marekani na Uingereza kutokana na nchi hizo kuliweka katika kundi la kigaidi.

Athari za uchaguzi huo ziligawa Palestina mara mbili na ndivyo inavyoonekana hadi sasa kutokana na tawala hizo mbili kukinzana.

**WAPALESTINA KUHAMISHWA?**

Hofu imetanda kuhusu nini kitafuata baada ya kumalizika kwa mapigano hayo Ukanda wa Gaza.

Wasiwasi ambao hata nchi zinazoiunga mkono Israel bado zinajitafakari kama baada ya vita hiyo mpango wa siri wa Israel wa kuwahamisha Wapalestina kama utatekelezwa.

Nyaraka za Uingereza zilizofichuka maajibu ya hofu zote kwa mpango huo miaka ya nyuma lakini haukutekelezeka.

Kulingana na BBC , nyaraka hizo zilizopatikana zinafichua kuwa Israel ilitengeneza mpango wa siri miaka 52 iliyopita wa kuwafukuza maelfu ya Wapalestina wa Gaza hadi eneo la Sinai Kaskazini.

Baada ya jeshi la Israel kuiteka Gaza, pamoja na Ukingo wa Magharibi, Jerusalem Mashariki na Miinuko ya Golan ya Syria, katika vita vya Juni 1967, Ukanda huo ukawa chanzo cha kero kwa usalama kwa Israel.

Kambi za wakimbizi zilizojengwa Ukanda wa Gaza ziligeuka kama maeneo ya upinzani dhidi ya walowezi wa Kiyaudi.

Kulingana na makadirio ya Uingereza, wakati Israel inaikalia kwa mabavu Gaza, kulikuwa na wakimbizi 200,000 katika Ukanda huo waliotoka maeneo mengine ya Palestina, wakifadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA). Watu 150,000 walikuwa wakazi asilia wa eneo hilo.

Ripoti hizo zilisema kwamba Gaza haikuwa na uwezo wa kiuchumi kutokana na matatizo ya kiusalama na kijamii yaliyosababishwa na maisha ya kambi na shughuli za Hamas.

Uingereza ilikuwa na wasiwasi kuhusu hali ya ardhi ya Palestina inayokaliwa kwa mabavu hususani Gaza.

Katika kujibu maswali ya bunge, serikali ya Uingereza iliarifu Baraza la Commons kwamba inafuatilia kwa uangalifu maendeleo katika eneo hilo.

Wakati huo huo, Ubalozi wa Uingereza nchini Israel ulifuatilia mienendo ya Israel ya kuwahamisha maelfu ya Wapalestina hadi Al-Arish, kaskazini mwa Peninsula ya Sinai ya Misri, takribani kilomita 54 kutoka mpaka wa Gaza na Misri.

Kulingana na ripoti za ubalozi huo, mpango huo ulijumuisha uhamisho wa kulazimishwa wa kwenda Misri au ardhi nyingine za Israeli.

Mapema Septemba 1971, serikali ya Israel iliwaambia Waingereza kwamba kulikuwa na mpango wa siri wa kuwahamisha Wapalestina kutoka Gaza hadi maeneo mengine, hasa Al-Arish nchini Misri.

Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano wa wakati huo wa Israel, Shimon Peres (Baadae Waziri Mkuu) alimweleza mshauri wa kisiasa wa Ubalozi wa Uingereza huko Tel Aviv kwamba wakati umefika kwa Israel kufanya zaidi katika Ukanda wa Gaza na kidogo katika Ukingo wa Magharibi. ”

Katika ripoti yake kuhusu mkutano huo, ubalozi ulisema Peres ambaye alikuwa na jukumu la kushughulikia maeneo yanayokaliwa kwa mabavu, alithibitisha kwamba ingawa serikali ya Israel haitatangaza rasmi sera hiyo mpya, wala haitachapisha mapendekezo ya kamati ya mawaziri.

Ripoti hiyo iliongeza kuwa Peres aliamini kuwa hatua hizo zitasababisha mabadiliko ndani ya nchi hiyo ndani ya mwaka mmoja.

Katika tathmini yake ya mpango huo wa siri wa Israel, Uingereza ilionyesha kwamba tawala za Mashariki ya Kiarabu ulitahadharisha kwamba chochote cha uhalali kwa sera hiyo, hawataweza kujizuia kuhisi kwamba Waisraeli wanaweza kupuuza.

**KWA MSAADA WA MASHIRIKA YA KIMATAIFA.**

SAFU

MAKALA

# KWELI FEDHA ZA UMMA MALI YA BIBI?



Na Magabilo Masambu

**Jambo baya zaidi ni kwamba asilimia kubwa ya wanaotajwa katika taarifa ile ni watu wanalipwa vizuri. Wakati fulani nashindwa kuelewa kwamba iwapo watu wanalipwa vizuri, iweje wanafanya ufisadi na wizi mkubwa kiasi hicho? Je, nini kinafanya watu hao kutochukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria? Je, dhambi hii ukomo wa ushirika wake ni wapi?**

BIBI katika jamii zetu ni mtu anayechukuliwa kama mtu mpole hasa kuhusu malezi ya Watoto hususani wajukuu. Vilevile kutokana na upole au upendo wake, hata mali yake ikichukuliwa hana kauli, pengine kwa sababu ya umri na kuishiwa nguvu ya kuipambania. Japo kwa bibi zetu wa zamani walikuwa wakali kwelikweli, tulichezea kipigo cha mbwa koko pindi tulipokosea. Baadhi walitumia mwiko kutandika au kufinya na vijiko mapajani.

Kama nchi tumekuwa na viongozi ambao hawana hofu tena na fedha za umma.

Zinachotwa kwa kadri ya uwezo wa wachotaji.

Haya yanathibitishwa na mjadala unaoendelea katika Bunge la 12 jijini Dodoma katika mkutano wa 13. Mjadala mzima umejikita kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Ukisikiliza maoni ya baadhi ya wabunge wetu ni kama wamebaki kulalamika na kwamba watalalamika kisha watanyamaza halafu mambo yatakwenda kama yalivyo. Wengine wamekwenda mbali zaidi, kupendekeza kuwapo na sheria za kunyonga wale wote watakaothibitika bila shaka kwamba wamefuja au kuiba fedha za umma. Kilio cha wabunge hawa kinaonekana kama kilio cha samaki majini na kwamba machozi yao yanabakia majini, hivyo hakuna atakaeyaona.

Ripoti ya CAG ya mwaka 2022 iliainisha maeneo mbalimbali ya ufujaji wa fedha za umma katika mashirika mbalimbali ya umma lakini kutokana na malalamiko ya wabunge, inaonyesha hakuna hatua madhubuti na za wazi, zilizochukuliwa dhidi ya wahusika waliotajwa kwenye ripoti hiyo. Kutokana na hali hiyo, ni wazi kuwa fedha za umma zinaweza kuchukuliwa kama mali ya bibi kwa sababu inaonyesha hakuna woga wowote.

Jambo baya zaidi ni kwamba asilimia kubwa ya wanaotajwa katika taarifa ile ni watu wanalipwa vizuri. Wakati fulani nashindwa kuelewa kwamba iwapo watu wanalipwa vizuri, iweje wanafanya ufisadi na wizi mkubwa kiasi hicho? Je, nini kinafanya watu hao kutochukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria? Je, dhambi hii ukomo wa ushirika wake ni wapi?

Nyakati za uchaguzi hakuna kiongozi anawaambia wananchi kwamba wamchague akajitengenezee maisha yake kwa kujilimbikizia mali za umma kupitia udanganyifu au wizi.

Kila anayeyataka madaraka anasema tumchague akapiganie maslahi ya wananchi wanyonge kumbe wanyonge wanakuja kunyongwa! Tuna kila sababu ya kupiga kelele kwa sababu tumepewa mamlaka hayo na Katiba ya nchi yetu. Kwa mujibu wa Katiba, tunapaswa kulinda rasilimali kwa manufaa yetu sote si kuneemesha baadhi ya familia, huku wengine wakiendelea kuishi kama watumwa.

Viongozi wanapata nafasi ya kusimamia tu rasilimali, si kuona kwamba wanayo haki ya kuzimiliki na kuzitumia kama zao.

Uzalendo unaohubiriwa haufanani na baadhi ya matendo ya viongozi wetu. Uzalendo ni pamoja na kutumia mali ya umma kwa manufaa ya watanzania wote, uzalendo siyo kuvaa bendera shingoni wala tai zenye rangi ya bendera, tunataka kuona uzalendo kwenye vitendo.

Kama jamii, tumekuwa na tatizo kubwa la kuwapamba na kuwaona mashujaa wanaotuibia huku wakiwa wamevaa suti na kalamu mikononi wakati vibaka wanaoiba kuku mtaani, tukiwaona hao ndio wezi na hatua za haraka kuchukuliwa. Siku hizi tunaowasifu kwa maendeleo ya haraka ni wale wenye nafasi ya kuiba mali ya umma na ikiwa hawataiba, tutawashangaa kwa nini wanafanya kazi muda mrefu bila kujenga na kununua magari ya kifahari.

Ushauri wangu kwa serikali, kwenye suala la wizi na ubadhirifu wa mali za umma, tusichague nani ashughulikiwe nani asishughulikiwe. Vinginevyo kama ufujaji huu ndio utakuwa msingi wa uendeshaji wa mambo, basi miradi mikubwa na midogo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi haitakamilika kwa wakati.

Serikali inatafuta pesa ama kupitia misaada au kukopa. Fedha hizo za mikopo zinalipwa na kila Mtanzania kwa njia mbalimbali kama tozo na kodi.

Kumbe tunafanya kazi ya kulipa fedha wanazozitumia wale tunaowaita wajanja! Jambo hili halitakuwa tofauti na unyonyaji aliyokuwa anaufanya mkoloni wa kuwatumikisha waafrika katika mashamba kwa ujira mdogo au wakati mwingine bure kabisa.

Maoni ya wabunge tunayasikia sote,.kuna haja ya kuchukua hatua kali kwa wale wote waliyohusika, vinginevyo hakutakuwa na sababu ya kuwepo ofisi ya CAG maana imekuwa kawaida kwamba kila mwaka watu wale wale wanatajwa na hatua hazichukuliwi.

Jambo hili litaleta tafsiri mbalimbali ambazo kwa kweli hazitakuwa nzuri kwa mamlaka za uteuzi za watu hao.

Tupige vita juu ya fedha ya umma kuonekana kama ni mali ya bibi. Hao hao wanaoiba fedha za umma si rahisi kuibiwa kama si rahisi kwao vipi kuhusu fedha za Watanzania?

**0689157789**
**Arusha-Tanzania**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Wasanii wataendelea kuwaponza walimu, ngoma zao hazina maadili*



Na Adam Fungamwango

**Tumeongea na wadhibiti ubora wapeleke taarifa kule, Mkurugenzi awaondoe walimu wakuu wa shule mbili, moja shule ya Tunduma na nyingine ambazo ni kama shule pacha, waondolewe madaraka ya ukuu wa shule watafutwe wakuu wengine wa shule. Tunafanya hivi ili kutuma ujumbe, walimu wakuu tusaidieni msiruhusu vitu kama hivi viingie shuleni," amesema Profesa Mkenda.**

VIDEO iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii inayoonyesha wanafunzi wa shule ya msingi wakicheza wimbo, wenyewe siku hizi wanaita ngoma ya msanii Zuchu imeleta mambo.

Video hiyo inayodaiwa kuwa ilirekodiwa Tunduma imemuibua Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, akaagiza Walimu Wakuu wa shule hizo wavuliwe vyeo.

Akizungumza Novemba 2, nje ya Bunge jijini Dodoma na Waandishi wa Habari, pia akapiga marufuku wanafunzi kucheza nyimbo zisizo na maadili na kuwataka walimu kuwa wasimamizi wa maadili pindi wanafunzi wawapo shuleni.

"Tumeshatambua shule yenyewe iko Tunduma, kulikuwa na kikundi kimeenda kutoa msaada shuleni pale, baada ya kutoa msaada ule kikaweka na muziki halafu wanafunzi wakacheza, na maudhui ya muziki wenyewe kila mtu ameusikia sina haja ya kuurudia.

Tumeongea na wadhibiti ubora wapeleke taarifa kule, Mkurugenzi awaondoe walimu wakuu wa shule mbili, moja shule ya Tunduma na nyingine ambazo ni kama shule pacha, waondolewe madaraka ya ukuu wa shule watafutwe wakuu wengine wa shule.

Tunafanya hivi ili kutuma ujumbe, walimu wakuu tusaidieni msiruhusu vitu kama hivi viingie shuleni," amesema Profesa Mkenda.

Nakumbuka mwaka jana hivi kuna video ilisambaa kama hivi ya wimbo wenye maneno ya ukakasi kama hivi ukipigwa kwenye basi la shule na watoto wakawa wanaimba kwa sauti, nao ulileta maneno kidogo.

Je, wanafunzi hawatakiwi kucheza? Hawatakiwi kufurahi? Siyo kweli. Hata huko zamani wanafunzi wa shule za msingi walikuwa wanaimba na kucheza nyimbo mbalimbali kwenye sherehe na mahafali, hata wakati wageni wanapozitembelea shule.

Kwa bahati nzuri nyimbo nyingi za zamani zilitungwa na kuimbwa kwa kuzingatia maadili. Na hata za mapenzi, bado hazikuwa na ukakasi wa maneno makali kama ya wasanii wa sasa.

Mfano wanafunzi wa zamani wakiwekewa wimbo hata wa mapenzi kama 'Georgina' au 'Rangi ya Chungwa', kutokana na maneno yaliyomo humo hayana matatizo yoyote.

Sidhani hata kama wale wanafunzi wangewekewa nyimbo hizo, wakaimba na kucheza, Waziri angejitokeza na kuagiza hivyo baada ya kuona video hiyo.

Sanasana tungevumbua tu vipaji vya waimbaji na wachezaji.

Shule za Msingi zinahitaji sana watoto wenye vipaji ili waanze utotoni, lakini si kwa nyimbo zenye maneno yenye ukakasi kama ule.

Hapa tayari walimu wanakwenda kuvuliwa vyeo vyao kwa sababu ya nyimbo za wasanii wa kisasa. asanii wasikwepe hilo. Watoto walikuwa lazima wacheze na kufurahi. Lakini wana nyimbo gani za sasa ambazo watazifurahia?

Nyimbo za wasanii wa sasa zote zinafanana tu maudhui. Asilimia 90 na zaidi ni mapenzi tu, na hata hayo mapenzi hayaimbwi, bali ni kutaja maneno yenye ukakasi ambayo mtu huwezi kukaa hata na watu unaowaheshimu. Je za maudhui mengine zipo wapi? Nyimbo za kufurahisha watoto nazo ziko wapi?

Je Zuchu mwenyewe anajisikiaje anaposikia wimbo wake umesababisha mtafaruku na kutajwa kuwa wimbo wake hauna maadili na usiwekwe kwenye sherehe za watoto? Yeye na wenzake wote inabidi wabadilike sasa.

Sawa wanaweza kuimba hivyo, lakini wajue pia hata watoto, wanafunzi nao wanataka nyimbo zao ili wafurahi.

Wawaige wanamuziki wa zamani ambao walikuwa na nyimbo za aina zote, matukio yote ya kijamii unayoyajua.

Ndiyo maana hadi leo kukitokea msiba wa mtu mkubwa au maarufu, nyimbo zinazotumika ni za Dr. Remmy Ongala.

Wanamuzikia wa zamani hawajaacha kitu, na hao watoto wangeweza kuwekewa wimbo wa Orchestra Safari Sound uitwao 'Pongezi kwako Mama', ambao unachezeka vizuri na mashairi yafuatayo.

"Natoa pongezi kwako mama, umenizaa na kunilea hadi nimekua. Unastahili pongezi mama, usiku kucha tabo nyingi umepata, usiku na mchana uko macho kunitunza, mapenzi yangu kwako mama hayana kifani ooo.

Sikusahau yoo yoo, baba na mama ni Mungu wa dunia, sikusahau yoo yoo, baba na mama ni Mungu wa dunia.

Ukiumwa kila siku njiani hospitali, sijui nikulipe nini mamaa, zawadi yangu ni kukulea, mpaka hapo Mungu atapokuchukua."

Kwa uchache tu, kuna wimbo wa 'Mama' wa Tancut Almasi, 'Msondo wa Nuta' wa Nuta Jazz, 'Chuma Chikoli Moto' wa OTTU Jazz na zingine nyingi ambazo zingejaa ukurasa mzima.

Wasanii wasidhani kama nyimbo za mapenzi tu au maneno ya kuoni ndiyo zinapendwa sana na watu, ikumbukwe Profesa Jay alitoa ngoma aliyoota 'Baba' ilipendwa na kila mtu hata Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli aliifagilia sana.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Kafie kwenu-18

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

GHAFLA aliona mtu anakuja kwa haraka. Akamtambua kuwa ni Catty. Akatabasamu. Akamuona akiwa anashangaashangaa. James akajiondoa kwenye kundi la watu na kumwita kwa jina, 'Catty!'

Kwa nusu dakika Catty alibaki akimshangaa aliyemwita. Kila akimwangalia anaona sura la James. Lakini si yeye.

"Ni mwenyewe au pacha wake?" Akawa anajiuliza kichwani. Akabaki haelewi nini afanye.

"Catty, ni mimi James, nimerudi!" Akajiweka wazi huku akitanua mikono wake.

Catty akakurupuka na kwenda kumkumbatia. Wote wawili machozi yaliwatoka. Lakini Catty akalia kwa sauti kama ilivyokuwa kwa Salma.

"Ni wewe kweli James. Au macho yangu yananidanganya?"

"Ni mimi. Ndiye James yule yule rafiki yako unayemfahamu. Nimerudi."

"Haa, James wewe ulikwenda wapi? Kwa nini hukutuaga, kuna watu tumehangaika hadi vituo vya polisi, hospitalini tumekusaka mpaka vyumba vya maiti..."

"Poleni sana, ni stori ndefu kidogo." "Kwani una haraka sana twende nyumbani ukapumzike kidogo."

James akamvuta kidogo Catty na kumnong'oneza jambo kwa sauti ya chini. "Angalia hapa kuna watu wengi sana wamekuja kunipokea wakiwemo watoto hawa rafiki zangu, nikija hatutoongea vizuri, wengine watabaki nje ya geti wakinisubiri. Nitakuja kesho usiku kama saa moja hivi bila mtu yeyote kujua, nadhani tutaongea vizuri."

Ndicho alichomnong'oneza. Catty akakubali, wakaagana. James akawaaga watoto, akawasha gari lake na kuondoka.

***********************************

"Hivi ni kweli mlinitafuta sana?"

"We James wewe, tulikusaka sana kama nilivyokwambia hadi vyumba vya maiti ili kama tupate walau mwili tuzike sisi majirani."

"Mlikuwa wangapi mliofanya kazi hiyo?" "Tulikuwa kama sita au saba hivi. Si unajua tena watu wa hapa hawakutaka kulipa uzito, lakini mimi nikahamasisha tukazunguka kote huko, mwenzangu tuliposhindwa kukuona, kuiona hata maiti yako, na hatumjui hata ndugu yako mmoja, basi tukashukuru Mungu. Kama umekufa basi Mungu akuweke mahali pema peponi, na kama upo hai basi akupe afya njema na mafanikio."




**"Enhe mwenzetu tuambie siri ya mafanikio yako, maana hatukuelewi ujue!" Catty akauliza swali ambalo nadhani kila mmoja anayemfahamu James angemuuliza. Hata mwenyewe James alilisubiri swali hilo haswa kutoka kwa mtu ambaye wanaelewana kama Catty.**

Ilikuwa ni sauti ya Catty akiongea kwa furaha na bashaha baada ya kumuona kwa mara nyingine rafiki yake James. Kumjali na kutomchulia kama ni mtu dhalili, kumheshimu na kutomnyanyapaa, ndiko kulikowafanya kuwa marafiki wakubwa na kama alivyomuahidi atarejea saa moja usiku alifanya hivyo.

Lakini safari hii hakuja na gari. Alikodisha bodaboda na kushukia mbali, akaja kwa miguu. Lengo ni kutofanya tena watu wajae kama ilivyokuwa mwanzo.

Wakati James akiingia nyumbani kwa kina Catty, Carry yeye alikimbilia chumbani na kujifungia kwa aibu.

Kila akikumbuka maneno yote aliyokuwa akimpachika mtoto wa watu anabaki na majuto moyoni.

Kwa sababu James ameridi kivingine siyo yule aliyoondoka, anaonekana sasa ana pesa ambazo hata hivyo hakuna mtu mwenye kujua nini kimesababisha arudi akiwa vile.

James akaangua kicheko kifupi, halafu akaongezea na maneno haya.

"Hilo la pili ndilo likafanikiwa, Mungu akanipa afya njema na mafanikio." Alipomaliza akatabasamu akimuangalia Catty kwa makini.

"Enhe mwenzetu tuambie siri ya mafanikio yako, maana hatukuelewi ujue!" Catty akauliza swali ambalo nadhani kila mmoja anayemfahamu James angemuuliza.

Hata mwenyewe James alilisubiri swali hilo haswa kutoka kwa mtu ambaye wanaelewana kama Catty.

Alimsifu alivyoliuliza kwa umakini sana. James aliendelea kumheshimu dada huyo kwani pamoja wameachana miaka mwili na nusu kupita, lakini kichwa chake bado kiendelea kuwa na hekima na busara, licha ya umri mdogo alionao kuliko dada yake. Akashusha pumzi. Tabasamu likaondoka kiasi cha kumtisha kidogo Catty.

Ndipo James alipomueleza Catty historia yote ya maisha yake, kuanzia mama yake Farida aliyekuwa hausigeli alivyopewa ujauzito na bosi wake mzee Joel Kamagi, kabla ya kutimuliwa kazi na yeye kuzaliwa miezi kadhaa baadaye ambapo waliishi maisha ya tabu uswahilini Vingunguti. Akaelezea mama yake alipofariki yeye ndiyo akaja kupanga kwenye kile kijumba kibovu chini ambacho walikuwa wanamuona anakaa pale jirani Kinondoni Moscow.

Akaeleza pia mzee Kamagi alikuwa ni mtu tajiri, na alikwenda kwa ndugu zake lakini walimtolea nje kuhusu mambo ya urithi.

"Nilikwenda hadi kwa ndugu zangu, lakini wakaniambia sitoweza kurithi mali za baba yangu kwa sababu mimi ni mtoto haramu, na kisa kile nilisababisha mama yao afariki dunia, basi nikarudi kuendelea kukaa hapa hapa, bila mtu kujua."

"Kumbe ndiyo hivyo. Sisi wote tunaishi na wewe hatujui maswahibu yaliyokupata. Pole sana James hizo ni changamoto wa maisha, na umeweza kuzivumilia kweli kweli."

"Ndiyo, ni kwa sababu ya usia wa mama yangu."

"Pole sana."

"Ahsante sana Catty."

"Enhee, sasa ikawaje?" Akauliza kwa sababu alijua hayajaisha. Yataisha tu pale atakaposikia stori ya nini kimebadilisha maisha yake.

"Siku moja niko hapa hapa nyumbani kwangu, usiku saa mbili, nilijiwa na wageni wawili. Mmoja namfahamu ni fundi wangu mkuu, mimi ni kibarua wake, na mtu mmoja mtu mzima kidogo hivi.

Yule fundi wangu akaniambia yule mzee alikuwa ananitafuta kwa muda mrefu, na kwa bahati nzuri walikutana sehemu na katika mazungumzo walinigusia, na kwa sababu mmoja ananifahamu hadi ninapoishi, akamleta.

Yule baba akaniambia alikuwa ananitafuta zaidi ya miezi sita tangu arudi masomoni. Alikuwa Ulaya kwa masomo ya Sheria, yeye ni Mwanasheria. Akaniambia yeye ni rafiki yake mzee Kamagi. Akasema kumbe kabla hajafariki aliandika urithi kwa watoto wake wote nikiwemo mimi. Mimi pia nina fungu langu kwenye mali na hisa za kampuni zake.

Aliandika na kumkabidhi yeye. Baba alishawahi kumwambia kuwa alimpa ujauzito hausigeli wake, wakamtimua kwa manufaa ya familia, na kwa miaka yote hajui wapi alipo kama alijifungua salama, au vipi. Ila akaandika urithi kwa mkono wake mwenyewe akamwambia kama Farida atakuwa amejifungua na mtoto wake yupo hai, basi na yeye awekwe kwenye urithi.


Baba akamwambia anaamini kama mtoto yupo hai basi ipo siku atajitokeza, na kama siku yeye akifa basi ameshaandika urithi wa mtoto huyo, akijitokeza na kuthibitika kuwa ni yeye, basi apate mgao wake wote. Ila alifanya hivyo kwa siri bila kuiambia familia yake kwa sababu hawakutaka mtoto yoyote wa nje arithi, lakini yeye hakutaka damu yake kama iko hai iteseke."

"He! Kumbe maisha yale yote ya ufukara baba yako alikuwa tajiri? Masikini weee."

"Ni kweli Catty, ila kama nilivyokueleza, mazingira hayakuruhusu, mama aliingilia ndoa ya watu."

"Du! Ila mzee alifanya kitu cha busara sana." "Ni kweli, ila kabla hata baba hajafariki, mzee huyo aliniambia yeye alikwenda Ulaya na huku nyuma baba akafariki dunia. Na kuchelewa kote kupata haki yangu ni kwa sababu yeye aliyepewa hati hizo hakuwepo nchini, ndiyo maana aliporejea na kukuta kifo chake, akaanza kunisaka kwa kuanza kuulizia watu taratibu hadi aliponipata." Catty alishindwa kusema lolote. Aliona kama ndoto hivi. Au hadithi za kufikirika.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# KUMBE NI MKALI

MAMA mzazi wa mwanamuziki wa Marekani, Beyonce, Tina Knowles ameeleza binti yake anapokuwa nyuma ya jukwaa wakati wa maonyesho, huwa na maneno makali.

Akizungumza na mwandishi wa habari, amesema licha ya tatizo hilo la mwanawe huwa na furaha na hahitaji tena kumuingilia kwa ajili ya kumsaidia kubadilika.

Amesema Beyonce anakuwa mkali wakati wa maonyesho yake, kiasi cha hivi karibuni alionekana nyuma ya jukwaa akimwambia kitu binti yake huyo.

"Majuzi nilipokuwa naye tulicheka kuhusu hili kwa sababu nilikuwa nikimwambia msichana, unakuwa mbaya sana huku nyuma,'" alimwambia mwandishi.

"Nina furaha sana kwamba sihitaji kurudi tena huko. Nataka tungecheka tu kwa sababu alikuwa akiigiza na akiimba eti mimi ni bibi msumbufu," alisisitiza.

Knowles alibainisha kuwa mwimbaji huyo mara nyingi alikuwa akiomba msamaha kwa tabia yake ya ukali akiwa nyuma ya jukwaa, hasa akikabiliana na shinikizo la maonyesho.

Beyonce majuzi alihitimisha ziara yake ya Renaissance, iliyoanza Mei 10, na ndiyo tamasha lililomuingizia pesa nyingi zaidi kwa msanii mweusi duniani.

# Harmonize azidi kumtaja Hamisa Mobeto



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Harmonize amesema Hamisa Mobeto ni aina ya mwanamke anayemtamani kuwa mke wake.

Akizungumza akiwa nchini Kenya, Harmonize amesema yeye na Hamisa wapo kama marafiki na kwamba ni mwanamke mrembo na kila mwanaume anatamani kuwa naye.

Hivi karibuni mwanamuziki huyo amekuwa akimtaja mrembo huyo kila wakati na baadhi ya posti zake amekuwa akimuhusisha kiasi ambacho kimeibua mjadala kama wawili hao wana uhusiano wa kimapenzi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RASHFORD AOMBA RADHI**
SHEREHE ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa ya Marcus Rashford saa chache baada ya Manchester United kufungwa mabao 3-0 na Manchester City "haikubaliki" na fowadi huyo ameomba radhi, amesema kocha Erik ten Hag.

**NEVILLE KUTUA MAREKANI**
KLABU ya Portland Timbers ya Marekani ipo katika hatua ya juu ya mazungumzo ya kumwajiri beki wa zamani wa England, Phil Neville mwenye umri wa miaka 46, kama kocha wao mkuu. Hapo awali alikuwa akiiongoza Inter Miami. (***Athletic***)

**NEWCASTLE YASAKA WAPYA**
NEWCASTLE United inamwania kiungo wa Atalanta na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Teun Koopmeiners mweye umri wa miaka 25, na beki wa kati wa Genoa na Romania, Radu Dragusin (21). (***Tuttomercatoweb***)

**VARANE ATAJWA SAUDIA**
KLABU kadhaa vya Saudia ikiwa ni pamoja na Al-Nassr zinatamani kumsajili beki wa kati wa Manchester United, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30, katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Teamtalk***)

**TADIBO AGOMBEWA ULAYA**
NICE imemwambia beki wa kati wa Ufaransa, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 23, iko tayari kumuuza mwishoni mwa msimu huu. Manchester United, Arsenal, Tottenham, Newcastle, Bayern Munich, Borussia Dortmund, Bayer Leverkusen, AC Milan na Atalanta zote zinammezea mate nyota huyo. (***90min***)

**SUAREZ KUMFUATA MESSI**
KLABU ya Inter Miami imefikia makubaliano na mshambuliaji wa Gremio na Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 36, ambapo ataungana na wachezaji wenzake kadhaa wa zamani wa Barcelona akiwamo Lionel Messi. (***ESPN***)

**ALCANTARA NJIA MOJA**
KIUNGO wa wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 32, anatarajiwa kuondoka Liverpool baada ya mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. (***Football Insider***)


**CITY YAMTAKA MAINOO**
KLABU ya Manchester City inamtaka kiungo wa kati wa Manchester United ambaye ni raia wa England, Kobbie Mainoo mwenye umri wa miaka 18. (***FourFourTwo***)

**MUSIALA KUBAKIA BAYERN**
BAYERN Munich ina uhakika wa kumsainisha kiungo wa kati wa Ujerumani, Jamal Musiala kwenye mkataba mpya huku Liverpool na Manchester City zikiwa na nia ya kumsajili ingawa mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 unaendelea hadi ifikapo mwaka 2026. (***90 min***)

**CANIO ALIIKATAA SAUDIA**
NYOTA wa zamani wa West Ham, Paolo di Canio mwenye umri wa miaka 55 amefichua alikataa nafasi ya kujiunga na kocha Roberto Mancini katika kikosi cha timu ya taifa ya Saudi Arabia. (***La Stampa, via Sun***)

**JEWEL ANUKIA RANGERS**
KLABU ya Rangers imemwendea ofisa mwajiri mkuu wa Brighton, Sam Jewell ambaye yuko nyuma ya wachezaji wakubwa waliosajiliwa na Seagulls. (***Star***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MARTINEZ: MBAPPE SHUJAA WA BAADAYE

**Kipa huyo wa Argentina amtabiria makubwa...**

**PARIS,** Ufaransa

GOLIKIPA wa Argentina, Emiliano Martinez anamwona mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe kama mshindi wa miaka ijayo wa tuzo ya Ballon dOr huku akieleza namna alivyoshindana na mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa wakati wa fainali ya Kombe la Dunia.

**Martinez alijikuta kwenye utata baada ya kuonekana akiwa ameshikilia mwanasesere mwenye uso wa Mbappe wakati wa gwaride la kusherehekea ushindi wa Kombe la Dunia mwaka jana.**

Aidha, inadaiwa pia aliwakusanya wachezaji wenzake kwenye chumba cha kubadilishia nguo baada ya kuifunga Ufaransa katika fainali ya Kombe la Dunia 2022 na kuimba wimbo ambao ulikuwa ukilenga kumpiga vijembe Mbappe ambaye alipachika mabao matatu dhidi yake kwenye fainali hiyo.

"Sio bure anachukuliwa kuwa mmoja kati ya wachezaji bora zaidi duniani. Ninamheshimu kama mchezaji na kama mwanaume," alisema akinukuliwa na jarida la L'Equipe baada ya kuchaguliwa kuwa kipa bora wa mwaka.

"Kylian ni mfano wa kuigwa. Ni mtu poa sana. Kushinda Kombe la Dunia, kucheza fainali ijayo na kufunga hat-trick. Wafaransa wote wanapaswa kujivunia kuwa na mchezaji kama yeye. Wakati Leo (Messi) na (Cristiano) Ronaldo watastaafu, Kylian atafuata njia zao."

Ingawa Mbappe alionekana kuchanganyikiwa baada ya kukosa tuzo, alionyesha kiwango chake kwa kutuma ujumbe wa 'unastahili' kwa Messi baada ya staa huyo kunyakua tuzo ya nane ya 'Ballon d'Or ambayo ilimfanya kuweka rekodi huko Paris.

# KOCHA WA MAMELODI AWASHANGAA AL AHLY



**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

KOCHA wa Mamelodi Sundowns, Rhulani Mokwena ameijia juu Al Ahly kwa kile alichokitaja kama "wanalalamikia kila kitu" baada ya Mafarao hao kudai mwamuzi aliwanyima penalti katika mchezo wa mkondo wa pili wa hatua ya nusu fainali ya michuano ya African Football League (AFL).

Al Ahly ilipoteza kwa matokeo ya jumla ya 1-0 baada ya kipigo cha 1-0 katika dimba la Loftus Versfeld, Pretoria Afrika Kusini kabla ya sare ya 0-0 kwenye marudiano jijini, Cairo.

"Nashangazwa sana na Al Ahly wanalalamikia kila kitu. Kabla ya mechi ya kwanza, Al Ahly walilalamika tulicheza saa 9:00 alasiri na bado walikuwa na uwezo wa kurekebisha mchezo kwa wakati unaofaa wakiwa kwao, lakini hautasikia malalamiko kutoka kwa Sundowns.

Kinachoshangaza zaidi Al Ahly huwa wanalalamikia waamuzi pale tu wanapopoteza. Jose Mourinho aliwahi kusema klabu kubwa inapoanza kutafuta sababu nyingine nje ya soka inaposhindwa basi ndio inaanza kupoteza hadhi yake ya kuwa klabu kubwa. Natumai sivyo ilivyo kwa Al Ahly kwa sababu ni kielelezo cha soka la Afrika.

"Baada ya malalamiko hayo ni nini hasa lengo lao? Kwa sababu ninaweza kupitia orodha ya matukio, ambapo waamuzi hawakufanya kile nilichofikiri ni haki kwetu. Mwishoni wa mechi, Sundowns ilifanya faulo saba na kupata kadi mbili za njano lakini Al Ahly walifanya faulo 13 na kupata kadi moja ya njano. Nadhani kama kuna timu ilipaswa kulalamika basi ilitakwa kuwa Sundowns." alieleza Mokwena.

Sundowns itachuana na Wydad Casablanca katika fainali ambapo mechi ya mkondo wa kwanza wa fainali itachezwa leo kwenye Uwanja wa Mohammed V, Casablanca kabla ya kurudiana Novemba 12, mwaka huu katika dimba la Loftus Versfeld ulioko Pretoria, Afrika Kusini.

Mshindi wa michuano hiyo mipya atapata kitita cha dola milioni nne na mshindi wa pili akitarajiwa kuchukua dola milioni tatu.

# Kichapo chamchefua Arteta

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta amesema amekerwa na kiwango cha timu yake kilichosababisha kuondolewa katika michuano ya Kombe la Ligi 'Carabao Cup'.

Arsenal ilikubali kichapo cha mabao 3-1 katika mchezo wa raundi ya nne ya michuano ya Kombe la Carabao, uliofanyika jijini London, England.

Arteta alifanya mabadiliko ya wachezaji sita katika kikosi chake cha kwanza huku mastaa Declan Rice, Bukayo Saka na nahodha, Martin Odegaard wakianzia benchi.

Arteta alisema amechukuzwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake na kusababisha kuondolewa katika michuano hiyo.

"Nimekasirishwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kiwango cha hali ya chini kilichoonyeshwa na wachezaji wa timu yangu.

Tumeondolewa kuendelea na michuano ya Kombe la Carabao kwa sababu mipango yetu ilikuwa kufika mbali zaidi.

"Baada ya bao la kwanza tulionekana kupoteza mwelekeo kitu ambacho siyo kawaida yetu, nina maumivu makubwa kufuatia kupoteza mchezo muhimu kwetu.

"Tunakwenda kujipanga kuhakikisha tunarejea katika ubora wetu na kufanya vizuri mechi inayofuata ya Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle United utakaochezwa kesho (leo)," alisema Arteta.



# Neville amwonya Ten Hag




**MANCHESTER,** England

GARY Neville amemwonya Erik ten Hag kuwa atafutwa kazi hapo Manchester United, huku Mholanzi huyo akikabiliwa na hatima ya watangulizi wake kwa sababu ameshindwa kuiwezesha timu hiyo kufanya vizuri.

United imetupwa nje ya michuano ya Kombe la Carabao baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-0 nyumbani kutoka kwa Newcastle United, mechi iliyochezwa Jumatano ikiwa ni siku tatu baada ya kupoteza mchezo dhidi ya Manchester City kwa idadi kama hiyo ya mabao.

Ten Hag sasa anashuhudia mwanzo mbaya zaidi wa msimu kwa United tangu msimu wa mwaka 1962-63 na klabu hiyo tayari imepoteza mechi tano kati ya 10 za nyumbani kwenye Uwanja wa Old Trafford ikiwa ni mara ya kwanza tangu mwaka 1930-31.

Neville alidokeza Ten Hag atatimuliwa United endapo timu hiyo itaendelea kufanya vibaya katika Ligi Kuu England pamoja na mashindano mengine.

United ilimaliza ya tatu katika msimu wa kwanza wa kocha huyo raia wa Uholanzi.

Beki huyo wa zamani wa kulia wa United ameonya mwenendo mbaya wa kocha huyo huenda ukamsababishia ajira yake ikafikia ukingoni.

Aidha, kocha huyo anasema pamoja na nafasi mbaya ilipo klabu hiyo, lakini yeye bado anaamini ndiye mtu sahihi zaidi wa kuiwezesha timu hiyo kufanya vizuri.

Ushindi huo wa mabao 3-0 ni wa kwanza mkubwa kwa Newcastle United ugenini dhidi ya Manchester United kwa miaka 93.

## HABARI MICHEZO

## JKT Queens kazini michuano ya CAF

**Na Saada Akida**

TIMU ya JKT Queens inatarajia kukutana na Mamelodi Sundowns Ladies katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Stade Amadou Gon Coulibaly ulioko Korhogo, Ivory Coast.

JKT Queens ambao ni mabingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), imepangwa Kundi A ikiwa pamoja na mwenyeji Athlético Abidjan, Sporting Club (Morocco) na mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns Ladies.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma alisema maandalizi yameenda vizuri na wanatarajia kuanza vyema michuano hiyo kwa kupata ushindi.

"Tutafanya vizuri, kila mchezaji amepewa majukumu yake, tunatambua tunakutana na timu kubwa ambayo inauwezo wa kupata matokeo makubwa mbele yetu lakini tutapambana," alisema Chabruma.

Kocha huyo alisema wamejipanga kucheza katika kiwango cha juu ili kuipeperusha vizuri bendera ya CECAFA na Tanzania kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

## *Simba SC, Yanga mechi ya kisasi*

INATOKA UK. 24

kuisaidia timu kupata ushindi.

Wachezaji wanafahamu mchezo huu umebeba hisia za mashabiki wengi, tutapambana ili kuwapa furaha, tupo tayari kwa mchezo,tunafahamu mchezo una presha kubwa na unabeba hisia kwa mashabiki na huwa unatazamwa sana, tumejiandaa kwa kila kitu kuhakikisha tunashinda na kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema Kapombe.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi alisema wamejiandaa vizuri na wanataka kushinda mchezo huo ambao anaamini utakuwa mzuri na utakaotawaliwa na mbinu.

Gamondi amewataka mashabiki wa Yanga waende kwa wingi kushuhudia mechi nzuri na amewaandalia furaha.

"Utakuwa mchezo wa tofauti sana,

# ZIMBWE JR AFUNGUKA, JOB ATARAJIA KICHEKO

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

WAKATI beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' akisema leo anatarajia kuweka rekodi ya kucheza mechi ya dabi ya 26 mfululizo, mlinzi wa Yanga, Dickson Job ametamba timu yake imejipanga kulipa kisasi kutoka kwa watani zao.

Zimbwe Jr aliliambia gazeti hili yeye ndiye mchezaji pekee mpaka sasa katika vikosi vyote viwili aliyecheza dabi nyingi zaidi na hali hiyo imemfanya asiwe na presha yoyote ya ndani ya nje ya uwanja.

Beki huyo ambaye alijiunga na Simba mwaka 2014 akitokea Kagera Sugar, tayari ameshacheza dabi 25 zikiwa ni za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA, Ngao ya Jamii na Kombe la Mapinduzi.

Alisema katika mechi zote za dabi alizocheza, hatosahau mechi tatu, moja ni ya kwanza kucheza katika maisha yake na ya pili ile iliyochezwa Oktoba Mosi, 2016 ambapo Amissi Tambwe alifunga bao baada ya kuushika mpira kwa mkono na Simba walirudisha kupitia kwa Shiza Kichuya.

"Kulikuwa na beki (jina hakulitaja) anacheza lakini majeruhi, wakati ule mwalimu alikuwa Patrick Phiri, akaniambia nijiandae kucheza na kwa bahati nzuri nafasi niliyopewa kucheza ndiyo hadi leo naishikilia, naendelea kuicheza, naendelea kuipambania," alisema beki huyo.

Aliongeza mara nyingi mechi za dabi hazihitaji mambo mengi zaidi ya kutuliza akili, kupambana na kujituma.

Naye Job alisema yeye pamoja na wachezaji wenzake wamejipanga vizuri kuhakikisha timu yao inavuna matokeo chanya.

"Naamini kutakuwa na ushindani, tutacheza kwa tahadhari kubwa kwa kushirikiana na wachezaji wenzangu. Bado tunaendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha, ninahafamu presha ya mchezo huo pindi timu hizi zinapokutana," alisema Job.

Nyota huyo pia amewashukuru mashabiki na wanachama wa timu yake kwa kuendelea kuwaunga mkono wakati wote.




Mwenyekiti wa Kamati ya Michezo ya Bunge, Festo Sanga (katikati), akizungumza kuhusu bonanza la wabunge ambao ni mashabiki wa timu za Simba na Yanga litakalofanyika Januari 27, mwakani jijini, Dodoma. Bonanza hilo litahusisha michezo 18. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Tanzania, Somalia kibaruani CECAFA*

**Na Adam Fungamwango**

YOSSO wa Tanzania wa umri chini ya miaka 15 wanatarajia kukutana na Somalia katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U1-5) itakayochezwa leo kuanzia saa 9:00 mchana kwenye Uwanja wa Njeru ulioko Jinja, Uganda. Mashindano hayo yalianza rasmi jana kwa Ethiopia kucheza dhidi ya Sudan Kusini na baadaye wenyeji Uganda waliikaribisha Djibouti.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, mchezaji wa timu hiyo, Ibrahim Ally alisema wamejiandaa vyema na michuano hiyo baada ya kupata maandalizi mazuri katika kambini yao iliyokuwa kwenye Kituo cha Ufundi cha TFF cha Mnyanjani, Tanga.

"Kikosi chetu kipo vizuri, tunashukuru sana kupata mazoezi ya kutosha, tulipata huduma bora, chakula, malazi na kufundishwa mbinu mbalimbali za kucheza mpira wa miguu, naamini sio kwenye mechi hii tu, bali tutafanya vyema katika mashindano yote," alisema nyota huyo.

Tanzania itashuka tena dimbani Jumatano kucheza dhidi ya Rwanda na itamaliza mechi zake za hatua ya makundi Novemba 11, mwaka huu kwa kukutana na 'ndugu' Zanzibar.

# Michezo

Jumapili Novemba 5, 2023

Nipashe




Neville amwonya Ten Hag

UKURASA 22



Ally Salim

Djugui Diarra

# Simba SC, Yanga mechi ya kisasi

## ●●● Robertinho, Gamondi kila mmoja atamba kuendeleza rekodi ili...

**Na Saada Akida**

WATANI wa jadi nchini, Simba na Yanga zote kutoka Kariakoo zinatarajia kukutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Timu hizo kongwe zinakutana ikiwa ni moja ya dabi kubwa tano Afrika kwa kipindi hiki, ikiwa ni mara ya pili wanakutana baada ya kucheza mechi ya ufunguzi wa msimu huu, wakimaliza dakika 90 bila kufungana na zilipokwenda hatua ya matuta, Simba ikaibuka mshindi wa taji hilo la kwanza la Ngao ya Jamii.

**Kuelekea mchezo huo, kila timu imekuwa ikitamba itaibuka na ushindi kutokana na kuwa na wachezaji bora ambao watawapatia matokeo chanya.**

Yanga itashuka dimbani ikiwa ndio vinara wa ligi hiyo na katika mafanikio yake, huwezi kuacha kuwataja wachezaji kama Stephen Aziz Ki, Maxi Nzengeli, Pacome Zouzoua na Yao Attohoula ambao wamefunga na kutoa pasi mabao.

Kwa upande wa Simba ambayo ina pointi 18 sawa na Yanga lakini imezidiwa mabao ya kufunga, tegemeo lake katika safu ya ushambuliaji inaongozwa na Kibu Denis ambaye amekuwa mwiba mchungu mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu kila wanapokutana katika siku za hivi karibuni.

Pia wapo Jean Baleke, kinara wa mabao ndani ya Wekundu hao wa Msimbazi akiwa na magoli sita huku Luis Miquissone 'Konde Boy' ameanza kupata 'moto' pamoja na Moses Phiri, wanatarajia kuibeba timu yao.

Nyota wawili wa Simba, Israel Mwenda na Aubin Kramo ambaye alifanyiwa upasuaji wa goti hawatakuwa sehemu ya mchezo wa leo dhidi ya Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' ameweka wazi wanaingia kwenye mchezo huo kwa lengo moja la kupambana na kupata pointi tatu muhimu.

Robertinho alisema siku zote timu kubwa lengo lake ni kupambana na kuhakikisha inapata ushindi katika kila mchezo na hilo ndilo Simba imejiandaa kulifanya kwa leeo.

"Ni kweli tunatarajia mchezo mgumu sana mbele ya Yanga kutokana na ubora wa kikosi chao, kama kikosi tunajivunia ubora wa maandalizi yetu kuelekea mchezo huu. Tumekuwa na michezo miwili mikubwa dhidi ya Al Ahly ambayo naweza kusema tulicheza kwa ubora mkubwa na tunapaswa kucheza katika kiwango bora zaidi ya kile ili kupata ushindi mbele ya Yanga, " alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema pia wanaiheshimu Yanga kwa sababu ni timu bora na siku zote dabi huwa haitabiriki lakini anatamani kuonyesha makubwa yeye na wachezaji wake kutokana na maandalizi imara waliyopata.

Aliongeza amekuwa akiamini mpira wa miguu unatakiwa kucheza vizuri na kushinda na hiyo ndio falsafa yake.

"Mechi ya dabi siku zote haitabiriki. Dabi inaamuliwa baada ya dakika 90 za mchezo, tunaiheshimu Yanga lakini tutaingia kwenye mchezo kwa lengo la kutafuta pointi tatu.

Ninawaamini wachezaji wangu, wana vipaji vikubwa na tumejipanga kushinda. Sina presha ya mechi ya kesho (leo), kama michezo mingine lakini kupata pointi tatu ndicho kipaumbele chetu," alisema kocha huyo.

Aliongeza kabla ya kuja Tanzania, amecheza dabi nyingi katika nchi alizofanya kazi na zote alifanya vizuri.

Beki wa kulia ni mchezaji mwandamizi Simba, Shomari Kapombe alisema wamepata maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na anaamini watatimiza majukumu yao na hatimaye kufikia malengo.

Kapombe alisema wiki moja waliyopata ya kujiandaa na mchezo huo mkubwa imetosha na wamedhamiria kupambana ili kupata ushindi.

"Mimi ni miongoni mwa wachezaji waliocheza dabi nyingi, nafurahi sana na inapofika siku kama ya kesho (leo), huwa sina presha, nahitaji kufanya vizuri ili

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >